**19 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 19 Juni, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Jesca Jonathani.

Na. 626

### Kupanda kwa Pensheni Kutokana na Mfumuko wa Bei

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, kwa nini Pensheni hazibadiliki na kupanda kutokana na mfumuko wa bei?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanda kwa pensheni hutegemea hali ya uhimilivu wa mifuko. Serikali hufanya tathmini ambayo matokeo ya tathmini hizo huwezesha kujua mifuko kama ni himilivu na ina uwezo wa kuhuisha pensheni za wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mafao, Serikali kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imepandisha kiwango cha Pensheni kutoka shilingi 100,000.00 hadi kufikia shilingi 150,000.00 kwa mwezi, kuanzia mwezi Januari, 2025, na pia kuhuisha pensheni kwa wastani wa asilimia mbili kwa kuzingatia mfumuko wa bei. Serikali itaendelea kuhuisha pensheni kadri uhimilivu wa mifuko yetu unavyoendelea kuimarika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Labda kwa maslahi ya wastaafu, kwenye bajeti ya 2026 pensheni hii imepandishwa zaidi kutoka shilingi 150,000.00 inafika mpaka shilingi 225,000.00 tulivyoelezwa jana. Nina maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Katika Mji wa Iringa tulikuwa tuna watendaji 25 waliokuwa wamejitolea na walipewa kibali cha kuajiriwa, lakini baadaye Katibu Mkuu aka-*stop* kwamba tusubiri, atatoa tena maelekezo mapya, mpaka leo hawajaajiriwa tangu mwaka 2024. Ni lini Serikali itawaajiri watendaji hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna mwalimu wetu mmoja wa kike anaitwa Rachel anayejitolea katika shule yetu ambayo iko mbali sana, na ni shule ambayo haina mwalimu wa kike kabisa. Huyu mwalimu amekuwa anafanya *interview* muda wote, kosa lake ni kwamba yeye ana *Degree,* lakini walimu

waliokuwa wanachukuliwa ni wenye *Diploma,* naye alikuwa tayari kujitolea, na amejitolea zaidi ya miaka nane katika shule hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kwamba inaweza kuwafanyia *consideration* ili aajiriwe moja kwa moja, kwa sababu shule hiyo iko katika mazingira ya mbali ambayo walimu wa kike wanashindwa kwenda kufundisha kule?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Moja, walimu wa kujitolea, kama utakumbuka vizuri, Waziri wa Utumishi alilitolea maelekezo na namna atakavyolifanyia kazi kwa wale watumishi wote ambao wanajitolea katika maeneo mbalimbali. Naomba tuendelee kuwa wavumilivu wakati Serikali inalifanyia kazi, kwa sababu ya uhalisia juu ya hawa watu ambao wanajitolea na kutoa michango mingi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili kuhusu nyongeza, *I mean* binti anayejitolea katika shule mojawapo katika mkoa wa Mheshimiwa Mbunge, hebu tulichukue, tutawafikishia watu wa Wizara ya Utumishi ili tuone namna nzuri ya kumsaidia binti huyu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Lambert, kwa niaba Mheshimiwa Matiko.

Na. 627

**Azma ya Ugatuzi wa Madaraka**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, ni maeneo gani ya kuweka mkazo ili Sekta nyingine zitekeleze na kuwa sehemu ya utekelezaji wa azma ya Ugatuzi wa Madaraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Ugatuzi wa Madaraka nchini inasimamiwa kupitia Andiko la Kisera la Maboresho ya Serikali za Mitaa la Mwaka 1998 *(Policy Paper on Local Government Reform, 1998)* na imelenga kupeleka madaraka, rasilimali na maamuzi kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida mbalimbali zimepatikana kwa kutekeleza sera hii ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa ushiriki wa wananchi katika kupanga, kusimamia na kutathmini maendeleo ya maeneo na kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii kwa umma, mathalan elimu na afya katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuharakisha suala la ugatuzi, Serikali imeandaa Rasimu ya Sera kamili ya Taifa ya Ugatuzi ambayo imeshaanza kujadiliwa katika ngazi mbalimbali za maamuzi, na pindi itakapokamilika na kuanza kutumika itaongeza ufanisi na kuimarisha ugatuzi katika sekta mbalimbali Serikalini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Sasa hivi kumekuwa na taratibu kutoka Serikali Kuu kwa baadhi ya Wizara kutaka kunyofoa idara mbalimbali ambazo kimsingi ziliwekwa kwa dhana ya Ugatuzi wa Madaraka. Kwa mfano, kumekuwa na matamanio ya kuondoa Maafisa Kilimo na Maafisa Ardhi kutoka kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuhalisia hizi ziliwekwa ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Sasa ninataka

kujua, ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba Wizara zote zenye matamanio ya kuondoa zile idara zisiondoe ili kuweza kuimarisha dhana nzima ya Ugatuaji wa Madaraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Sera ya Kikodi ambayo kimsingi inazitaka Serikali za Mitaa kukusanya mapato yote na kuzipeleka Hazina, halafu ndiyo zirejeshwe kwa ajili ya operesheni mbalimbali za Serikali za Mitaa, zimekuwa zikitatiza kwa sababu kwanza, hazirudi kwa wakati, lakini wakati mwingine zinarudi kwa upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba zinaimarisha na kuhakikisha fedha zote ambazo zinakusanywa kupelekwa Hazina zinarudishwa kulingana na bajeti na makadirio ya Serikali za Mitaa, na kwa wakati ili kuweza kuimarisha utendaji wa shughuli wa kila siku katika Serikali za Mitaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa misingi ya Ugatuzi wa Mdaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa umewekwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 145 na Ibara 146.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kujua umuhimu na msingi mzima wa dhana hii ya Ugatuzi wa Madaraka, kama nilivyotangulia kujibu katika majibu ya msingi, tayari imeshafanya hatua za kimsingi kabisa za kutengeneza Rasimu ya Sera Kamili ya Taifa ya Ugatuzi, na ipo katika hatua mbalimbali za majadiliano na kupitiwa ili mwisho wa siku iwe sera kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha sera hii, kuimarisha dhana hii ya Ugatuzi wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Esther Matiko, amezungumza kuhusiana na baadhi ya Wizara za Kisekta kuwa na matamanio ya kuhamisha Maafisa, mathalani Maafisa wa Kilimo; Maafisa wa Ardhi, kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwarudisha katika uwajibikaji moja kwa moja kwenye Wizara zao. Kazi kubwa na *component* muhimu ya Ugatuzi wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na kuwa na mahusiano kati ya Serikali Kuu na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kazi yake mojawapo ni ku-*coordinate* au kutengeneza huo muunganiko wa sera zinazosimamiwa na Wizara za Kisekta katika utekelezaji huku kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na jitihada hizo ili kuendelea kuimarisha dhana hii kwa maana hata Hayati Baba wa Taifa aliweka msisitizo mkubwa sana katika uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuelezea umuhimu mkubwa sana wa ugatuzi kwa lengo la kuhakikisha kwamba wananchi ndio wanafanya maamuzi, wanashiriki moja kwa moja kwenye kupanga, kusimamia na kutathmini maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia upande huu, sera ikikamilika itaendelea kuimarisha katika upande huu na kwa sasa hivi tayari mafunzo yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na suala la pili, Mheshimiwa Esther Matiko amezungumza kuhusiana na Ugatuzi wa Fedha *(Fiscal Decentralization)*, ambayo na yenyewe ni *component* muhimu sana katika Ugatuzi wa Madaraka *(D by D)*. Serikali katika eneo hili inaendelea kuimarisha kwa kuziwezesha Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kuwa bunifu kuibua miradi ambayo itaweza kuziwezesha mamlaka zetu kukusanya mapato ili ziweze kupanga maendeleo yake na kutekeleza maendeleo kwa ajili ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zinaimarika kimapato, zinaweza kuwa na hiyo *Fiscal Decentralization* ambayo wote tunatamani ifikiwe ili ziweze kuimarika. Mahusiano kati ya fedha zinazotoka Serikali Kuu ambazo zenyewe kimsingi zinakuwa ni kwa ajili ya ku-*supplement* (kuongeza nguvu) katika kazi na wajibu wa msingi wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ya kukusanya mapato na kupanga maendeleo, itaendelea kuimarisha pia upande huo kwa maana ya Serikali Kuu iweze kuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, fedha ziwe zinafika kwa wakati kwenye mamlaka zetu ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Serikali itazingatia hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ili kufanikisha Ugatuzi wa Madaraka ambapo Serikali imefanya kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, tunahitaji kuwa na wataalamu wa kutosha katika mamlaka hizi. Je, ni kwa kiasi gani uhaba wa wataalamu, kwa mfano Wahandisi umeathiri ufanisi wa Ugatuzi wa Madaraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu mkubwa sana wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu, utekelezaji wa Sera mbalimbali za Kisekta, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba, kunakuwa na wataalamu wa kutosha kwenye hizi Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kwa ajili ya *backstopping*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba inaajiri wataalamu mbalimbali. Ukiacha tu Wahandisi ambao Mheshimiwa Prof. Ndakidemi amewataja, lakini

wataalamu katika sekta mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wa msingi wa *backstopping* kuwa na ile *technical assistance* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu na kwamba Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zinakuwa na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na jitihada hizo kupitia Wizara ya Utumishi. Kila mwaka wanaajiriwa watumishi wa kada mbalimbali kwa ajili ya kupangwa katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa ili mamlaka zetu hizi ziweze kuwa na huduma nzuri kwa kuwa na wataalamu ambao wanasaidia katika utekelezaji wa majukumu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Mwakasaka kwa niaba Mheshimiwa Sekiboko.

Na. 628

**Ukosefu wa Huduma ya Umeme Vitongoji vya Tabora Mjini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua tatizo la kukosa huduma ya umeme katika Vitongoji vya Jimbo la Tabora Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Mjini lina jumla ya Vitongoji 159 ambapo kati ya hivyo, vitongoji 69 vimepatiwa umeme, vitongoji 15 Wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa miradi kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Kwanza, na vitongoji 24 zabuni imetangazwa ili kupata Wakandarasi wa kutekeleza miradi kupitia Mradi wa Kupeleka

Umeme Vitongojini Awamu ya Pili. Vitongoji 51 vilivyosalia vitapelekewa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa bado malalamiko mengi kwamba umeme unavyopelekwa kwenye vitongoji, majengo ya kutolea huduma kama hospitali, shule, na miradi ya maji, bado inakuwa hayajapelekewa umeme, je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba umeme unapofika kwenye kitongoji moja kwa moja unafika kwenye majengo ya kutolea huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kupeleka umeme kwenye vijiji na vitongoji katika maeneo yetu, je, ni upi mkakati wa kuhakikisha kwamba ile bei ya kuingiza umeme ya shilingi 27,000.00 inarejeshwa katika maeneo mengi ili kuwapa wananchi nafuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yamekuwepo malalamiko kwamba, baadhi ya maeneo yenye huduma muhimu huwa yanasahaulika kupelekewa umeme wakati umeme unapopelekwa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wote Serikali imesisitiza kwamba kipindi kile ambapo *survey* zinafanyika, ni vizuri viongozi wa maeneo yale wakahusika, wakashirikiana na wakandarasi kuyabaini maeneo yale ili yaweze kuingizwa kwenye maeneo ambayo yatahakikishiwa yatapata umeme wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linaposhindikana kufanyika, matokeo yake tunakuta tunapata hii changamoto. Kwa hiyo, rai yangu ni kwa viongozi kwenye maeneo yetu, wawe makini wakati ule wahandisi wanapokuja kufanya *survey,* basi waweze kushiriki ili kuainisha maeneo muhimu yasijeyakaachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hili la bei, kama tulivyosema tangu awali, msingi wa bei hii ni kutambua maeneo kwa mujibu wa taratibu zetu za Kiserikali yanayoainishwa kwamba ni maeneo ya vijijini. Pale ambapo maeneo hayo kwa bahati mbaya yamesahaulika, Serikali tupo tayari kupokea ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na mamlaka zilizopo kule kwenye halmashauri ili maeneo haya yaweze kuingizwa kwenye utaratibu wa kulipa bei hii ya shilingi 27,000.00.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mwakamo, kwa niaba Mheshimiwa Issaay, ngoja. Mheshimiwa Dkt. Kimei umesimama kwa niaba au?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Haya, endelea.

Na. 629

**Tofauti ya Gharama za Kuingiza Umeme Majumbani – Kibaha Vijijini**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI K.n.y. MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza: -

Je, zipi sababu za kuwa na gharama tofauti ya kuingiza Umeme majumbani Kibaha Vijijini badala ya kuwa na bei moja ya shilingi 27,000.00 tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetofautisha gharama za kuunganisha umeme kulingana na eneo husika ambapo kwa maeneo ya vijijini, gharama za kuunganisha umeme ni shilingi 27,000.00 na kwa maeneo ya mijini yakiwemo maeneo ya Miji Midogo gharama ni shilingi 320,960.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo la Kibaha Vijijini, Kata za Kwala na Dutumi ni maeneo yanayopakana, vijijini hivyo vinalipa shilingi 27,000.00 kama gharama ya kuunganisha umeme. Aidha, maeneo yanayopatikana katika Kata za Mlandizi, Mtongani, Kawawa, Janga, Kikongo, Kilangalanga, Boko na Soga ni maeneo ya Mji Mdogo, hivyo wateja wa maeneo hayo wanalipia shilingi 320,960.00 kama gharama ya kuunganisha umeme.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, Serikali inaonaje umuhimu wa kuchukua mikopo kwenye taasisi mbalimbali ili waweze kuwafungia wananchi ambao hawana uwezo wa kulipa kwa mkupuo mmoja shilingi 320,000.00 mpaka 350,000.00, halafu baadaye wakaweka kwenye gharama za kutoa umeme kwa hawa wateja wakawa wanalipa kidogo kidogo? Je, Serikali inasemaje kuhusu hoja hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Serikali inaunganisha umeme kwa wananchi wengi, jitihada mbalimbali zimechukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, tumepiga hatua kubwa ya kuhakikisha kwamba vijiji vyote nchini vimeweza kuunganishwa na umeme, na sasa tunakwenda kwenye eneo la vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maarifa yoyote yatakayotuwezesha kuhakikisha kwamba tunawaunganisha wananchi wetu kwa ukubwa na kwa ukamilifu, Serikali itayaangalia kuona uwezekano wake wa kutekeleza na pale inapoonekana inawezekana, tutafanya hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Oran Manase.

Na. 630

**Ujenzi wa Barabara ya Mchepuko ya Mlima Nyoka**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mchepuo ya Mlima Nyoka kutoka Uyole hadi Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshaanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Mlima Nyoka kutoka Uyole hadi Songwe yenye urefu wa kilometa 48.9 ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi ikiwemo utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi *(PPP)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa, Bandari yetu ya Dar es Salaam inafanya vizuri, na magari ya mizigo ikiwemo ya mafuta yameongezeka sana kwenye barabara hiyo ambayo inapita katikati ya jiji, je, sasa ni lini wananchi waliopisha ujenzi wa hiyo barabara wakiwemo wa Kata ya Inyala, Kata ya Ijombe, Kata ya Swaya, Kata ya Igale, Kata ya Lwindi na Kata ya Bonde la Songwe watalipwa fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kipande cha kilomita 22 wa barabara ya Isyonje – Kikondo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Oran Njeza kwa maswali yake ya nyongeza mawili ambayo ameyauliza ambayo kimsingi yanasadiki umuhimu wa barabara yetu hii kubwa katika kusaidia Bandari yetu ya Dar es Salaam na kuinua sekta ya uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza kuhusiana na upande wa fidia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo, uthamini umekamilika kwenye barabara ya Mbeya *bypass* na tayari tumeshaanza kulipa fidia. Tumelipa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya wananchi wa maeneo hayo. Hivyo, nawaomba wananchi wote wanaonisikiliza wa Kata alizozitaja ikiwemo Kata ya Ijombe, Swaya, Igale, Lwindi na Songwe kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha na inao mpango wa dhati wa kuwalipa fidia ili wapishe eneo hilo au eneo hilo liende kutumika kwa ajili ya barabara yetu ambayo tumeizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumza kuhusu jambo la pili barabara ya Isyonje – Kikondo kilomita 22 hadi Makete kwamba ni lini pengine ujenzi wake utakamilika? Nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama tunavyofahamu mpaka sasa Serikali imekamilisha ujenzi wa kilomita za lami zaidi ya 12,000 na katika Awamu ya Sita peke yake; miaka minne zaidi ya asilimia 10, zaidi ya kilometa 1,300 barabara za lami zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kutokana na umuhimu mkubwa wa barabara hii aliyoizungumza, inayounganisha Mikoa miwili katika Mkoa wa Njombe pamoja na Mkoa wa Mbeya, tayari usanifu wa kina umeshakamilika na ujenzi umeshaanza kuanzia kwenye Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape matumaini wananchi wa Mbeya na watu wa mikoa yote hii miwili na maeneo mengine kwamba tunakwenda kujenga barabara hiyo kama ambavyo tumekuwa tukiwaeleza, kwa sababu tayari kazi imeshaanza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Swali Namba 632, Mheshimiwa Eng. Manyanya kwa niaba Mheshimiwa Mbunda.

Na. 632

**Uhitaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Nyasa**

**MHE. JONAS W. MBUNDA K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, lini Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litakuwa na Ofisi ya kuendesha shughuli zake katika Wilaya ya Nyasa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi kwa kujenga vituo vya zimamoto na uokoaji. Katika mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imetenga kiasi cha fedha shilingi bilioni 6.4 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo cha Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji katika Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Nyasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitoe shukrani kwa Serikali kwa kutenga fedha hizo kwa ajili ya kujenga ofisi na maeneo ambayo vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vinafanyia kazi. Ninataka nijue, katika Wilaya ya Mbinga, je, kiasi hiki kilichotengwa kitahusisha na Wilaya ya Mbinga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wilaya ya Mbinga ni sehemu ya wilaya zitakazonufaika na mpango huu, na hivyo nikutoe wasiwasi kwamba Wilaya ya Mbinga ni miongoni mwa wilaya ambazo zitapitiwa na mradi huu kwa sababu ni *operation* ya nchi nzima kuhakikisha Wilaya zote tunazipelekea huduma ya majengo ya zimamoto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutuletea Askari wa Zimamoto Wilayani Lushoto, lakini Askari wale walioletwa hawana hata vitendea kazi kama vile gari la zimamoto. Je, lini Serikali itapeleka gari la zimamoto na vitendea kazi vingine ili kuokoa matukio yanapotokea ya moto kwa wananchi wetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba vifaa vya zimamoto hapa nchini yakiwepo magari vinasambazwa pote nchini. Nilipokuwa nikijibu swali kama hili jana, nilieleza mpango wa Serikali juu ya ununuzi wa vifaa ambavyo vinahusisha magari karibu 100 ambayo yatapokelewa hivi karibuni hapa nchini, na matarajio yetu yatasambazwa katika wilaya zote hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Shekilindi kwamba Wilaya yake haitabaki nyuma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ninakushukuru kwa kuwa hii siyo Wizara yako, lakini umejibu kwa usahihi kabisa. Umeonyesha ukomavu wa Serikali hii na Waheshimiwa Mawaziri wetu mnavyofanya kazi vizuri sana. Hongereni sana.

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Zuwena Bushiri kwa niaba Mheshimiwa Festo aulize swali.

Na. 633

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Arusha Chini - Moshi Vijijini**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, lini skimu ya umwagiliaji itajengwa katika Kata ya Arusha Chini Moshi Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu mbalimbali nchini, ikiwemo Skimu ya Umwagiliaji ya Chemiko yenye ukubwa wa hekta 2,000 iliyopo katika Kata ya Arusha Chini Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2025/2026 itakamilisha usanifu wa skimu hiyo na kuanza taratibu za manunuzi ili kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi. Kukamilika kwa ujenzi wa skimu hiyo, kutaongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula nchini na hivyo kuwanufaisha wakulima wa Kata ya Arusha Chini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sababu ni katika kipindi hiki Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika sekta ya umwagiliaji. Hii ni kuonyesha kwamba Serikali imekusudia kufanya mapinduzi kwenye sekta ya kilimo. Nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, wananchi hawa wa Kata ya Arusha Chini wamekuwa wakisubiria sana hii skimu kuanza, kwa sababu kama unavyojua, Arusha ni moja kati ya mikoa ambayo uzalishaji wa mbogamboga ndiyo unaoendesha maisha ya kila siku. Sasa wanaiuliza Serikali, ni lini wataanza kuijenga skimu hii ili wananchi waweze kupata fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Ni kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Makete Kata ya Mfumbi Skimu ya Mwamlenge tumewaomba shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa skimu hii ili iweze kufanya kazi kwa hekta 520. Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizi ili wananchi hawa waweze kupata maji na kufanya kazi kwenye skimu hii katika uzalishaji wao wa shughuli za kiuchumi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Festo Sanga kwa maswali yake ya kizalendo. Mapinduzi katika sekta ya kilimo hakika yapo bayana. Tuna kila sababu ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, vilevile kumpongeza Mheshimiwa Waziri Bashe pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa Silinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, mwaka huu upembuzi yakinifu umefanyika na mwaka ujao wa fedha 2025/2026 tunatarajia tuweze kukamilisha kazi hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye Skimu ya Mwamlenge katika Jimbo lake, mara Serikali itakapokamilisha taratibu zote hizi, skimu zote tunazitarajia mwaka ujao wa fedha ziweze kujengwa. Lengo kubwa ni kuendeleza mapinduzi ya kilimo na kuhakikisha wakulima wote nchini wananufaika na kazi nzuri inayofanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jackson Rweikiza, yupo mwenyewe, yule pale. *(Makofi)*

Na. 634

**Kilimo cha Mazao ya Alizeti na Mawese Kagera**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, lini Kilimo cha Mazao ya Alizeti na chikichi kitaanza Mkoani Kagera kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais akiwa Bukoba Juni, 2022?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukuza kilimo cha mazao ya alizeti na chikichi katika Mkoa wa Kagera, Serikali kati ya mwaka 2021 na 2025 imesambaza jumla ya miche ya michikichi 15,840 katika Mkoa wa Kagera ili kuimarisha uzalishaji wa zao hilo. Pia, miche ya chikichi 2,908 inaendelea kutunzwa katika vitalu vya *TARI* - Maruku kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima wa zao la chikichi katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imehamasisha wakulima katika Mkoa wa Kagera kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti kutoka tani 2,716.64 mwaka 2023 hadi tani 3,047 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 12.16%.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi hii au agizo hili alilitoa Mheshimiwa Rais mwaka 2022. Tulikuwa tumeomba hivi kwa sababu bei ya kahawa ilikuwa duni sana, ilikuwa shilingi 900.00 kwa kilo, sasa hivi bei ya kahawa ni shilingi 5,100.00. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupigania zao la kahawa limekuwa zao la kiuchumi na zao zuri sana. Sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hana swali. Haya amepongeza, ni kweli haya ndiyo mambo tunataka. Mambo yakifanywa na Mheshimiwa Rais

na Serikali yake yasemwe humu ili wananchi wasikie na watu wajue na kazi inayofanywa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Mwanyika, karibu uulize swali lako.

Na. 635

**Mradi wa Maji Kata ya Uwemba – Njombe Mjini**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Maji Kata ya Uwemba – Njombe Mjini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ununuzi wa kumpata Mkandarasi atakayetekeleza Mradi wa Maji Kijiji cha Uwemba uliopo Njombe Mjini. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 300,000, ulazaji wa mtandao wa bomba umbali wa kilometa 49.8, na ujenzi wa vituo 12 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi huo unatarajia kuanza mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2025/2026 na utakuwa kwa muda wa miezi nane. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naishukuru sana Serikali kwa mradi huu ambao tumeungojea kwa muda mrefu sana. Ni habari njema sana kwa watu wa Mtaa wa Uwemba. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa maji utategemea chanzo cha maji kinachotoka kwenye milima ya Madope katika

Wilaya ya Ludewa. Ili mradi ufanye kazi, ni lazima ni kile chanzo kifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa hivi, bomba la kwenda kuunganisha na hicho chanzo lipo tayari, lakini kuna mradi mwingine mkubwa wa barabara ambao umevuruga lile bomba katika baadhi ya maeneo. Sasa swali langu ni je, Serikali inaweza kutoa maelekezo mahususi ili mkandarasi yule ambaye anashughulika na lile bomba au barabara arudishie bomba kwenye maeneo hasa ya Kata ya Luponde maeneo ya Madope ili mradi ule ukikamilika kule maji yaweze kupita? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba changamoto moja ilikuwa ni fedha, lakini sasa kwa sababu tayari bajeti imeshapitishwa, tumeshaidhinishiwa fedha takribani shilingi trilioni 1.06, sasa zinakwenda kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ni kwamba nataka nitoe maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* na viongozi wanaohusika na hili, kwa sababu haliwezekani mradi huu ukwame kwa sababu ya ujenzi wa barabara ambao umechukua muda mrefu. Ninawaelekeza na kuwasisitiza na kuwaomba sana wanaosimamia *TANROADS,* wahakikishe kwamba hili jambo linakwenda kukamilika ili mradi ukamilike na wananchi waweze kupata huduma kwa wakati. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, maswali yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Jijini Dodoma ambao ni Wakurugenzi wa Utawala; Ndugu Maimuna Kiruu, Ndugu Mary Abdallah, Ndugu Susan Okayo, Ndugu Evangelina Luchabala, Ndugu Hidaya Ally, Ndugu Chiratina Kimalo. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 62 wa Mheshimiwa Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii,

Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambao ni watoto na Watumishi wa Makao ya Taifa ya Watoto, Kikombo kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Kikundi cha *Goreeb Foundation* kutoka nchini Uingereza. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ambao ni Ndugu zake kutoka Kilolo Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rwekiza, Ndugu Amani Moshi, ni mpiga kura wake kutoka Mkoani Kagera.

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mhadhiri na Mtafiti wa Masuala ya Lishe na Kinga wa Chuo Kikuu - KCMC kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Ndugu Mercy Urio ambaye ni mpigakura wake kutoka Arumeru Mashariki, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Ndugu yake kutoka Makete Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Ndugu Rajab Ramadhan ambaye ni Kijana wake kutoka Ofisi ya *Star City* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, wadau wa maendeleo kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, ni watoto wake kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Edwin Swalle, ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari ya Kingdom Heritage kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu, wapiga kura wake kutoka Singida Mashariki wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Tadayo, ni wasanii wa filamu kutoka Mwanga Mkoani Kilimanjaro. Hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, ambao ni rafiki zake kutoka Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 58 wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwanza ni wanafunzi 71 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi Yakin kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 111 na walimu 14 wa Shule ya Awali ya Msingi *Little Treasures* kutoka Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni wetu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**na**

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Tadayo, wajiandae Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa na Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwa asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ameniongoza katika kipindi chote hiki cha Bunge la Kumi na Mbili ambalo sasa linaelekea mwisho kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninakishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kupeleka jina langu kwa wananchi mwaka 2020 ili nipeperushe bendera ya Chama Cha Mapinduzi kwa nafasi hii ya Ubunge. Ninaamini kabisa nimekitendea haki chama changu katika dhamana ambayo walinipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru zaidi wananchi wote wa Jimbo la Mwanga kwa kunipokea nilipoletwa na Chama Cha Mapinduzi na kuniamini na kunipa dhamana ya kuwawakilisha kwa nafasi hii ya Ubunge. Ninaamini kazi hii imefanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwataarifu tu kabisa kwamba tunaelekea mwisho wa kuchukua fomu, na mimi niko njiani ninakwenda kuchukua fomu na ninaamini kabisa kwa kazi ambayo Mungu ametuwezesha kufanya, basi watakuwa tena na imani ya kuweza kunirudisha siyo mimi tu, hata wewe kule Jimboni Ilala, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumekaa vizuri sana humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake makini. Kwa kweli wananchi wa Mwanga wameona kazi ya Mheshimiwa Rais, Tanzania imeona na hata dunia imeona na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais amepewa tuzo *awards* nyingi sana katika kipindi hiki, kwa sababu dunia imeona kazi ambayo amewafanyia Watanzania na ameifanyia dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiye mtu sahihi wa kupeperusha bendera ya CCM na kuendelea kuliongoza Taifa hili kwa kipindi hiki kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiwe mchoyo wa fadhila, ninamshukuru sana Mheshimiwa Spika pamoja na wewe na viongozi wetu wote wa Bunge kwa jinsi ambavyo mmetulea hasa sisi Wabunge wa Awamu ya Kwanza, mkatuongoza tukaweza kufanya kazi zetu kwa viwango hivi ambavyo tumefanya. Tunawashukuru mmetujengea uwezo mkubwa sana wa kuweza kutupa *confidence* ya kurudi kwa wananchi kusema tupeni tena kipindi kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopita ilitekelezwa vizuri sana. Tumeona kwenye taarifa kwa viwango vikubwa vya zaidi ya 90%. Hii inadhihirisha kwamba viongozi wetu waliotuongoza katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Naibu wake ni viongozi sahihi kwa sekta hii. Kwa hiyo, tunaweza kuwaamini kabisa na kuiamini pia bajeti ambayo

wameileta kwamba itatuvusha. Bajeti hii iko vizuri, na mimi niseme mwanzoni kabisa kwamba ninaiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi ninaitazama bajeti hii kama bajeti ambayo imelenga kuondoa utegemezi kiuchumi kwa kuchochea zile sekta muhimu za uzalishaji na kupanua wigo wa kodi na kuweka pia mifumo rafiki kwa ajili ya kukusanya kodi. Kwa hiyo, ni bajeti ambayo imeanzia pazuri, kwa vile ile iliyopita ilitekelezwa vizuri kiasi ambacho tumeona kwamba uwiano wa deni na pato la Taifa ni 20% wakati ukomo ni 40%. Hilo ni jambo zuri na hata mashirika yenye hadhi kubwa Kimataifa kama *MOODY'S* yalipokuwa yanatufanyia tathmini, yametutathmini kwamba bado tuko vizuri, na hivyo kufanya hata deni letu liwe himilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee mbele kwa ujasiri bila hofu na bila kusikiliza maneno mengi. Tufanye kazi kwa moyo na kwa kujiamini kwa sababu kweli tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona mapunguzo ya kodi katika maeneo mbalimbali ambayo ni nyeti kama vile maeneo ya kilimo, utalii, madini pamoja na uendelezaji wa rasilimaliwatu. Kwa upande wa kilimo ninapongeza kuondoa kodi ya ongezeko la thamani katika viuatilifu. Hii itasaidia wakulima kuweza kulima vizuri zaidi na kuondoa *VAT* kwenye nguo zinazotengenezwa na pamba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo litachochea sana wakulima wa pamba kuendelea kufanya vizuri na kupata kipato na hiyo sekta kukua kwa kasi pamoja na maeneo kama ya mbolea, mafuta ya kula yanayotengezwa kwa mbegu zinazolimwa hapa nchini, matairi ya trekta pamoja na vipuri mbalimbali. Hizo ni hatua nzuri za kusaidia kukuza zile sekta za muhimu ambazo tunaziangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia kwenye madini na gesi, bajeti haikuwasahau wale watu wadogo wadogo wa bodaboda ambayo ni ajira kubwa, kwani nimeona pia kuna

unafuu wa kodi kwenye badoboda, yaani katika maana ya pikipiki, bajaji, pamoja na guta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguzwa kwa *Hotel Levy* pamoja na bima ya wageni, pia ni jambo la muhimu sana ambalo litachochea sekta hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia upunguzaji wa kodi kwenye magazeti yanayotengenezwa humu ndani. Hii pia ni hatua nzuri katika kuwafanya watu waendelee kupata taarifa na pia kuweza ku-*exercise* demokrasia kwa sababu demokrasia pia inahitaji haki ile ya kupata taarifa na kutoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza na kusisitiza sana kwamba tasnia nzima ya habari pamoja na sanaa iweze kupatiwa nafuu mbalimbali. Pia, urahisishwaji wa masharti yao ya usajili na kulinda kazi zao kwa sababu sanaa na habari ni ajira kubwa, lakini pia ni kiungo muhimu sana katika kutimiza haki ya kidemokrasia ya kutoa na kupata taarifa, jambo ambalo ni muhimu katika uchumi wa nchi inayokua kama hii ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa pia na suala la kudhibiti uholela wa wageni kufanya kazi ambazo zinapaswa kufanywa na wenyeji. Kwa kweli ni aibu tunapoona wageni wanafanya kazi za *screen printing,* ku-*print t-shirt* kule Kariakoo, na kuuza vitu barabarani. Hii kwa kweli imekuwa aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwamba sasa tumeamua aibu hii tuachane nayo. Sisi wenyewe tukienda huko nje tunafuata masharti ya kufanya kazi; siyo kwamba mtu aje hapa na ukiangalia vyeti vyake labda amekuja kama mhandisi, lakini anauza *tiles* barabarani. Hii siyo sawa sawa. Suala hili ni muhimu sana, Serikali ikatae watu wa namna hii ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lipo jambo moja ambalo aligusia rafiki yangu Mheshimiwa Byabato jana kuhusu hili sharti

kwamba lazima mwekezaji akifungua kampuni kuwe na hisa fulani ambazo zinashikiliwa na wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamekuwa na mtindo kwamba ikishaandikwa pale kwenye *Memorandum and Articles* ukienda anakuonyesha hii hapa, utakuta labda ni mhudumu wake wa ndani au dereva wake au *messenger* pale ofisini amempa zile *shares.*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatakiwa kwa kweli twende hatua mbele zaidi kwa sababu *shares* zinazoandikwa kwenye mtaji ambao kampuni inaruhusiwa kufanya biashara *(Memorandum and Articles* ile ni *authorized share capita*l). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka twende chini zaidi tuone *he should share capital,* kwamba ni *share* ngapi zimekuwa *issued* kwenye ile kampuni na *paid share capital?* Tuone yule ana-*share certificate,* amelipia kodi na baadaye tumwone kwenye *minutes* akiingia kwenye vikao na akishiriki kwenye maamuzi na kupata d*ividend* mwisho wa mwaka, na kodi ilipwe, ndiyo tutakubali kweli huyu ni mwanahisa; lakini hii habari ya kuchomekachomeka watu tu pale siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi tu jimboni kwangu Mwanga, kwa kweli niseme wazi kwamba katika Awamu hii ya Sita, jimbo la Mwanga limetendewa haki. Miradi yote ile ya kimkakati ambayo ilikuwa kwenye ilani na ambayo tuliomba baada ya ilani, imetekelzwa. Kuna iliyokamilika kabisa, lakini kuna iliyo kwenye hatua nzuri za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama Mwanga, tunasema ilani imetekelezwa, Serikali imetutendea haki, na Mheshimiwa Rais ametufanyia haki. Kwa hiyo, hatuna mashaka na tunachokisema kwamba yeye ndio mtu sahihi wa kuendeleza kupeperusha bendera ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nzima inafahamu kwamba kulikuwa na mradi mkubwa sana wa maji wa Same – Mwanga –

Korogwe. Mradi umekamilika sasa mwaka wa 19 huu toka umeanza, lakini Mheshimiwa Rais ameufungua, tunakunywa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekamilisha *masterplan* ya Mji wa Mwanga ambayo ilikuwa na *package* ya miradi; Hospitali ya Wilaya, *VETA*, barabara ya kimkakati ambayo tumeita *CD Msuya Bypass,* jengo la utawala la halmashauri pamoja na stendi. Hivyo, kuna ambavyo vimekamilika na vingine viko kwenye hatua nzuri za kiutekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa siwezi kumaliza mambo yote, lakini ukienda tu kwenye elimu, tumejenga madarasa 139, tumejenga shule mpya tano za sekondari na za msingi kadhaa, tumejenga mabweni 19, tumepandisha hadhi Chuo cha Ustawi wa Jamii kuwa Chuo Kikuu Kishiriki, tumejenga lango la utalii sasa, tunafaidi matunda ya hifadhi ya Mkomazi na tumepata miradi mikubwa ya umwagiliaji, wa mwisho ukiwa ni mradi wa shilingi bilioni 16.894 na ni mradi mkubwa sana ambao utatupunguzia sana kero ya suala la ajira, kipato na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, siyo huo peke yake; kuna mwingine wa shilingi bilioni 4.8 na mwingine wa shilingi bilioni 1.064. Si jambo la mchezo, kwa kipindi kifupi ambacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekaa madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kimsingi, sisi mambo yako vizuri, lakini yako mambo tu matatu ambayo ni ya kukumbusha. Ninasema ni ya kukumbusha kwa sababu yameshaanza utekelezaji na mengine Mheshimiwa Rais alishayatolea maelekezo. Kwa mfano, stendi ya kisasa katika Mji wa Mwanga, bajeti ilishapita na tumeshaandaa uwanja. Kwa hiyo, ni suala tu tunaomba fedha zile ambazo ziliahidiwa zije pamoja na kituo cha afya cha kimkakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, mradi wa kuondoa magugumaji ya Ziwa Jipe ambazo pia

bajeti ilishatengwa. Tunaomba Wizara ya Fedha sasa; hili hatumwambii tena Mheshimiwa Rais, tunaiambia Wizara ya Fedha, tunaomba tukamilishe hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Ezra, halafu wajiandae Mheshimiwa Chaurembo, na Mheshimiwa Jesca.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2025/2026 ambayo *in fact,* tuseme ndiyo hotuba yangu ya mwisho katika Bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kipekee niwashukuru sana wananchi wa Biharamulo walionipa ridhaa ya kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka hii mitano ambayo tunaimalizia. Kwa niaba yao, nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama Kiongozi Mkuu wa Serikali na Kiongozi wa nchi kwa miradi mingi ya heshima ambayo ametupatia watu wa Biharamulo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri hii juzi Jumatatu nilikuwa jimboni nikafanya nao mkutano wa kueleza ni mambo gani yamefanyika. Kwa hiyo, yote wanayo, wanayajua. Tuzidi kuishukuru Serikali na tukitarajia katika bajeti hii ambayo tunaipitisha sasa, lakini na Ilani ya CCM ambayo tayari imeshazinduliwa, waliokabidhiwa wagombea wetu kwenye mkutano uliopita tunaamini tutapata ushindi wa kishindo kwa haya tuliyoyatekeleza na tutatekeleza yale ambayo tumeahidi katika ilani mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa sababu bajeti hii kwangu mimi nimesema kwamba ni bajeti ambayo imegusa maisha ya wanyonge na watu wa chini kabisa

ambao kiasili walisahaulika kwa muda mrefu. Jambo la kwanza, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake ya Awamu ya Sita kwa ongezeko la mishahara ya kima cha chini cha wafanyakazi wa nchi hii kwa 35.1%. Hili ni ongezeko kubwa na la kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini tunaposema mambo mazuri haya yanafanyika, hata wale waliokuwa wanyonge wakilipwa kidogo, wamelipata ongezeko na wameliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutakuwa mashahidi, tumemsikia Waziri wa Fedha na kitabu chake cha bajeti hapa kimesema, hata wastaafu wanaolipwa kutokea hazina pensheni zao waliokuwa wanapokea shilingi 100,125.9 kwa mwezi na sasa imeongezeka, imeenda shilingi 250,125.9. Hili ni ongezeko kubwa sana kwa wastaafu, hivyo tuzidi kuishukuru Serikali kwa kuwaona. Tunaamini hakitoshi, lakini kitasaidia kusukuma maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukisoma katika Sheria ya Kodi ambayo kwenye kitabu chetu cha bajeti ni sura ya 332, Serikali imetangaza unafuu wa kodi ya mapato kwa bajaji na pikipiki. Pikipiki zikitoka shilingi 65,000.00 mpaka kuwa zero, lakini bajaji na baiskeli zote za miguu mitatu zikitoka shilingi 120,000.00 na kuwa sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni unafuu mkubwa sana, ndiyo maana nikasema hii ni bajeti ambayo imegusa maisha ya watu wa chini kabisa. Wote tunajua maisha yetu na hasa familia zetu za kimaskini na za Kitanzania, tumekuwa tunabebwa na watu wa bodaboda na ndiyo ajira kubwa iliyoko kwenye familia zetu na maeneo yetu. Kwa hiyo, tunapoona Serikali inawagusa na kuwakumbuka kwamba hata wao wapatiwe unafuu wa maisha hasa katika kodi, ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaipongeza Serikali, kwani wakati Waziri wa Fedha anawasilisha hotuba yake hapa alisema dhahiri kabisa kwamba katika bajeti hii wanaelekeza biashara za

watu zisifungwe, bali kuwe na *dialogue* kati ya taasisi zinazo-*control* biashara na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini hili jambo limesikika kwa muda mrefu, nadhani watu walikuwa wanasema halijawahi kutolewa maelekezo na Serikali. Sasa kwa sababu Serikali imetoa maelekezo *vividly* ndani ya hili Bunge, tunaamini hiki kitu kitatekelezwa na sasa itasimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi unaposema mfanyabiashara, dereva wa bajaji ni mfanyabiashara; na dereva wa bodaboda au pikipiki ni mfanyabiashara, maana ndicho kinachompa kipato na ndiyo maana alikuwa *considered* hata katika habari ya mapato. Sasa tuombe kupitia Bunge hili, na hasa Serikali inapoenda kumalizia majibu, tupate majibu ya uhakika kwa sababu tunachokipitisha hapa ni kwamba Serikali imeelekeza wafanyabiashara wasisumbuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua dereva wa bajaji au bodaboda maisha yake na biashara yake ni pikipiki. Pale anapokosea ukamnyang'anya leseni, maana yake umemfungia biashara kwa sababu hawezi tena kufanya biashara; na hawa watu wanalea familia na ndiyo hao wanaotunza familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuombe kuwe na *dialogue* kuanzia kwa watu hawa wa chini wa bodaboda, na watu wa bajaji. Hata anapokosea, suala la kumnyang'nya leseni na kumfungia leseni, Serikali imeeleza, tuwe na *dialogue,* atafutiwe adhabu, lakini asikatishwe *cashflow* ya familia yake kwa sababu huyu mtu anatunza familia, anasomesha, na vitu vingine. Unapomtoa barabarani, kama alikuwa anaendesha bodaboda ya mtu, na yule mtu akamnyang'anya, inamharibia kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninasoma katika kitabu chetu cha bajeti ukurasa wa 108, Sheria ya Kudhibiti Uingizaji wa Bidhaa Ndani ya Nchi Sura Na. 276. Ninaishukuru sana Serikali, nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa miaka hii mitano, na katika kitu ambacho tulikuwa tunaomba

sana, Serikali ikifanyie *consideration,* ni *protection* ya wazalishaji wa ndani katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba kunakuwa na *tariffs* za *HS Code* na nini huwezi kuongeza *import duty* au kufanya mpaka mkubaliane, lakini *introduction* au kuviweka hivi vitu vingi ambavyo vimeenda kwa kuweka kwenye kitengo kinachoitwa tozo ya maendeleo ya viwanda, imetusaidia mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongea kwa habari ya mabati *ALAF,* sasa hivi wamefungua kiwanda kikubwa, na Kamati yetu ilitembelea pale. Kwa hiyo, *introduction* ya tozo kwenye *HS code* hizi kwa 15% itasaidia sana uingizaji wa mabati yanayotoka nje, tulinde viwanda vyetu vya ndani. Pia, tumeona hata viwanda vya nondo, Kamati yetu ilitembelea kiwanda cha Ruvia, nilisema tunatengeneza mpaka *BS500* zinazalishwa hapa. Zamani tulikuwa tuna-*import* hizi nondo, lakini leo zimezalishwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nondo nyingi zilizotumika kwenye mradi wa *SGR* zimezalishwa hapa nchini. Kwa hiyo, kitendo cha kufanya *protection* kama hii, itasababisha uwekezaji mkubwa ndani ya nchi. Licha ya uwekezaji, itasababisha ajira ndani na mapato ya watu wetu yataongezeka *rather than* pale ilipokuwa inazalishiwa kule nje, tunakuwa tu soko la kupokea bidhaa ambazo zimeshazalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaipongeza Serikali kwenye haya yote, maana nilikuwa napitia ukurasa wa 108 mpaka ukurasa karibu wa 110, mambo mengi ambayo tuliyaomba yamekuwa *considered*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria hii ya Kodi ukurasa wa 108(2) inasema, "kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 10% kwenye vichwa vya *trailer* vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS code* zimetajwa hapo." Hii ndiyo *case* ambayo nilitaka niongee kidogo, na ninadhani Waziri wa Fedha angenisikiliza vizuri hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika hii nchi, vichwa vya *trailer* tunafanya *importation.* sasa tunapoongeza hii kodi ya maendeleo ya viwanda *why?* Sisi hatuzalishi vichwa vya *trailer, what are we bring in the market now*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, hii itasababisha usafirishaji uwe mgumu kwa sababu, unapoongeza 10% na wenzako hawajaongeza 10% kwa kuwa hivi vichwa tunavi-*import.* sisi sio watengenezaji wa *Volvo, Howo* na vitu vingine. Tunachotengeneza ni *trailers,* lakini vichwa vinakuwa *imported,* vichwa tayari vina-*import duty,* vina *VAT* na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba, pamoja na kwamba tuna nia nzuri ya kuongeza mapato, hili jambo tuliangalie, litaumiza Watanzania wengi kwa sababu, wasafirishaji wataongeza hizi gharama na anaenda kuzibeba mtu wa mwisho. Sisi tunaotoka bara huko, mbali kutoka Dar es Salaam kwenye bandari, kilometa zaidi ya 1,400 unafika Kagera, hii itatuumiza. Maisha yatapanda sana kwa sababu ya usafirishaji. Kwa hiyo, tuombe hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua tunahitaji kodi, lakini tusiumizumize hawa watu. Kama sehemu nyingine tumetengeneza unafuu, Mtanzania wa mwisho tunayemtengenezea unafuu ndiye huyu aliyeko huko mikoani kwa sababu, tuna ujenzi wa madarasa na tuna ujenzi wa vitu vingi; tutahitaji mizigo isafirishwe kutoka kwenye viwanda vingi ambavyo viko Dar es Salaam kufika bara kwetu huku. Hii bajeti ya ujenzi ambayo imepangwa na vitu vingine, bei zitapanda kwa sababu ya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei zitakapopanda, maana yake ni hata bajeti itakuwa *distorted.* Kwa hiyo, tuombe hili tujaribu kuangalia, kama mnaweza mkapata chanzo kingine, hii 10% ya maendeleo mnayoongeza kwenye vichwa vya *trailer* vinavyokuwa *imported* kwa sababu, *what are we protecting?*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu anayezalisha vichwa vya *trailer* hapa kwamba, tungekuwa tuna *alternative* humu

ndani. Kama kuna mtu angekuwa anazalisha, una *alternative, is well,* unam-*protect* mtu wa ndani ili anayeingiza aweze kupata shida, lakini sasa tunaenda kupandisha kila kitu. Aliye na ma-*trailer* ya zamani kwa sababu wafanyabiashara ndio wale wale, anayeingiza mapya atapandisha tu bei *automatically*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingiza soko kwenye *distortion* kubwa na wananchi wanaenda kuumia, *especially* tunapopokea bidhaa huko nje. Kwa hiyo, tuombe hili mlione, kama mnaweza mkafanya *consideration* ya *adjustment* ya kutafuta hela kwenye vipengele vingine, bado tuna nafasi. Ndiyo maana tunajadili muswada huu. Hili tuliona tuwapunguzie wananchi mzigo ili tuweze kupunguza hii gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, kwa mara nyingine tena nashukuru. Nakushukuru wewe mwenyewe binafsi na ninamshukuru sana Spika wetu wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati ambao wamekuwepo hapa pamoja na viongozi wengine kwa ushirikiano mlionipa kwa miaka hii mitano. Ninaamini kilikuwa ni kipindi changu cha kwanza cha kujifunza. Mungu akisaidia tutakaporejea, tutarejea na nguvu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu atusaidie wengi tuliomo humu, kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunayo ya kujivunia majimboni na tunayo ya kwenda kusema. Tusiwe waoga, tunyanyuke kishujaa, turudi majimboni, tukawaambie wananchi, tumefanya nini kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais? Ninaamini wananchi ni wasikivu, Watanzania wameona yaliyofanyika, watatupa ridhaa nyingine tena. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca, na Mheshimiwa Dkt. Rweikiza jiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, ambaye kwa kipindi hiki cha miaka mitano tunachomaliza, ameendelea kunitunza, kunipa afya njema na kunipa weledi mkubwa wa kuweza kujadili mambo mbalimbali ambayo yamekuwa yakiwasilishwa hapa Bungeni na hasa katika suala zima la kuwasilisha changamoto na kero zinazowakabili wananchi wangu wa Jimbo la Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi, CCM, kwa kipindi chote cha miaka mitano, kimenipa ushirikiano mkubwa sana. Kimenikumbusha mambo mengi ambayo yalikuwa yameahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mbagala, wameweza kunipa nafasi kubwa ya kuchangia. Sikuweza kupata usumbufu wowote katika wakati wangu wa uongozi wa kipindi cha miaka mitano; wamenipa ushirikiano mkubwa na wamenipa hoja za msingi za kuweza kuzungumza hapa Bungeni. Ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naishukru sana Serikali. Hoja zangu zote nilizoziwasilisha hapa Bungeni, zikiwepo kero za wananchi wangu wa Jimbo la Mbagala, Serikali yetu sikivu pamoja na Mawaziri wake wote wamenitekelezea kwa asilimia kubwa. Ninawashukuru sana, *inshallah,* Mwenyezi Mungu atawalipa na Mheshimiwa Rais pia, atamlipa kila lililo la heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kutoa shukrani zangu kwa Serikali kwa miradi mikubwa ambayo imefanyika katika jimbo langu. Katika sekta ya elimu, msingi peke yake katika kipindi hiki, haijawahi kutokea, shule tisa mpya zimejengwa katika Jimbo langu la Mbagala, na pia, shule za sekondari nane mpya zimejengwa. Jimbo langu la Mbagala lilikuwa halina *high school,* sasa hivi zimejengwa mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana viongozi wote wa Serikali kwa kuniletea Shule ya Mchepuo wa Kiingereza katika Jimbo langu la Mbagala. Ninaamini katika suala la elimu, Jimbo la

Mbagala sasa hivi tunatembea kifua mbele, lakini pia, niendelee kushukuru, vituo vya afya vitano vipya, vimejengwa katika Jimbo langu la Mbagala pamoja na hospitali kubwa mbili za wilaya zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishukuru sana Serikali katika suala zima la barabara. Fidia ya shilingi bilioni 16.8 ambayo ilikuwa kero kwa muda wote imetekelezwa, na watu wamelipwa. Kikubwa zaidi, naishukuru sana Serikali chini ya Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa suala zima ambalo lilikuwa kero; suala la X zilizowekwa kutoka Rangitatu - Mbande mpaka Mongola. X zile baada ya kuleta hoja zangu hapa Bungeni, zilifutwa na wananchi sasa wanaendelea na taratibu zao, hawana bugudha. Huko tunakokwenda tumeanza kuomba upanuzi wa barabara ile na hatimaye ikikubalika barabara ile kupanuliwa, wananchi wale watalipwa fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi imetekelezeka kwa asilimia kubwa. Ukisoma kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho mambo yaliyokuwa yameahidiwa katika Jimbo la Mbagala yametekelezwa. Kwa hiyo, ninaendelea kuishukru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu vya bajeti vyote tulivyokuwa navyo, yale yote ambayo yameandikwa katika jimbo langu yametekelezeka. Nimeyataja baadhi, na kwa sababu ya muda, siwezi kuyataja yote. Tunayo Ilani Mpya ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, vile vitu ambavyo vimebaki, vidogo vidogo, vyote vimewekwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kukishukuru sana Chama cha Mapinduzi, kwa maana yale yote tuliyokuwa tukiyawasilisha na wao wameendelea kuyafanyia kazi. Kikubwa zaidi, ukichukua kitabu cha bajeti ambayo ndiyo tunaijadili na kuipitisha hii leo, yale mambo yote ya msingi yaliyobaki, zikiwepo barabara za Mtaa wa Dovya, Mwapemba, Kwa Mfindi, Vigoa, Kwa Kashikashi, Kwa Mwarabu, kwa Mzungu na Kilamba hadi Mashine ya maji zimeandikwa katika kitabu hiki. Ndiyo maana sina

sababu ya kutokuiunga mkono bajeti hii kwa maana sisi watu wa Jimbo la Mbagala tunashukuru sana, yale yote tuliyoyaomba yameweza kutekelezwa na mengine yapo katika kitabu cha bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumshukuru Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, wakati akitoka Dar es Salaam kuelekea Rufiji alisimama pale Mbagala. Baada ya kusimama Mbagala, pamoja na michakato mbalimbali tuliyokuwa tukiifanya katika halmashauri ya kuomba Jimbo letu la Mgagala likatwe, tuliomba tena Mheshimiwa Rais baada ya kumweleza tuliyoyafanya na michakato mbalimbali. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, jambo letu la Jimbo la Mbagala kukatwa, limekatwa na sasa tumepata Jimbo jipya la Chamazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa Watu wa Mbagala na Chamazi yapo mambo ambayo tunatakiwa tujiulize. Kama jimbo lilipokuwa na Mbunge mmoja maendeleo yamepatikana kwa kiasi hiki, je, sasa hivi yamepatikana majimbo mawili? Ninaamini maendeleo yatakuwa makubwa zaidi ya haya yaliyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii sasa kuwaambia Wanambagala, mimi kama Mbunge wao, kwa kuwa makazi yangu yapo katika Jimbo Jipya la Chamazi, kwa hiyo, ninawaambia nitagombea katika Jimbo la Chamazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawatoa hofu wale wote waliokuwepo katika Jimbo la Mbagala, Bunge hili ni la Kitaifa. Tunajadili mambo ya nchi nzima. Kwa hiyo, zile changamoto zilizokuwepo katika Jimbo la Mbagala ambalo ninaenda kuliachia, nitaendelea kushirikiana na Mbunge anayekuja kuhakikisha tunaendelea kutatua changamoto hizo. Wale marafiki zangu nawatoa hofu, tutaendelea kushirikiana nao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza hiyo, lakini nina mambo mawili machache ya mchango katika bajeti hii. Jambo la kwanza, tumeendelea

kuipongeza Serikali, lakini kiukweli Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kutibu magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni jukumu letu Wabunge tuipunguzie mzigo Serikali kuwatibu wagonjwa wa magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza kwa kutoa elimu na ushauri kwa wananchi wetu kubadilisha *life style* tunazokwendanazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia magonjwa ya moyo, shinikizo la damu, kisukari na kansa, haya siyo magonjwa ya kuambukiza, lakini yanatokana na *life style* zetu tunazoishi. Ninaomba nichukue nafasi hii kuwaomba Wabunge wenzangu, *inshallah* Mwenyezi Mungu atatudisha hapa Bungeni, muda wetu mwingi tukiwa majimboni, mwakani tuwaelimishe wananchi wetu ili waweze kuepukana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ambayo yatailetea faida kubwa nchi yetu kwa kutokutumia fedha nyingi, kwa ajili ya kuwatibu wagonjwa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusafisha damu. Wabunge wengi hapa tuliomba gharama za kusafisha damu zishushwe, lakini tumeshindwa kuona ni namna gani ambayo tunaweza tukawashauri wananchi wetu wakaepukana na matatizo yanayotokana na magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwahamasisha wananchi wetu kuepukana na magonjwa ya kuambukiza, tafsiri yake, ni hatutakuwa na sababu ya kuona sasa namna gani ya kuiomba Serikali ipunguze gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kusafisha damu kwa mgonjwa mara ya kwanza anapofika hospitali ni shilingi laki saba, lakini kila wiki anatakiwa atumie zaidi ya shilingi laki tatu, mara mbili au tatu kwa wiki, ni gharama kubwa. Tutakapoendelea kuwashawishi wananchi, maana yake ni kwanza wao maisha yao yataendelea kuboreka, kwa maana watakuwa hawatumii fedha nyingi kwa ajili ya matibabu, lakini la pili, tutaipunguzia mzigo Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa wale ambao wanapata misamaha, katika zile shilingi 300,000.00 Serikali inachangia shilingi 120,000.00; hebu tuangalie mzigo mzito ambao tunaikabidhi Serikali. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge wenzangu, tuwashauri na tuwaelekeze wananchi wetu kufanya mazoezi pamoja na kubadilisha maisha yetu, ili tuepukane na magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la ardhi. Ninashukuru, tunaenda vizuri, lakini zipo changamoto kwenye ardhi, changamoto ambazo zinasababisha Serikali kutumia gharama kubwa wakati wa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka mitano, hapa tumekuwa tukizungumzia suala la fidia, fidia, fidia, lakini kama tungepima maeneo yetu vizuri, leo hii tungekuwa hatuzungumzii suala la fidia, kwa sababu, maeneo yote yangekuwa yamepimwa. Maeneo ambayo tunataka kujenga barabara yangekuwa hayana tena changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nikutakie kila la heri na wewe kwenye Jimbo lako la Ilala. Nimtakie kila la heri Mheshimiwa Spika kwenye jimbo lake jipya na niwatakie kila la heri Wabunge wote tuliopo hapa kwa kazi kubwa tulizozifanya. Ninaamini watakaobaki ni wale wenye roho mbaya kwa sababu, roho mbaya haina dawa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca. Jiandae Dkt. Rweikiza na jiandae Mheshimiwa Kisau.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kusimama leo katika Bunge hili Tukufu. Kwa kweli, kusimama kuchangia bajeti hii kwa mara ya mwisho ni wakati wa kumshukuru pia Mwenyezi Mungu. Nachukua

nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na mtume ambaye alisema, kupitia Kitabu cha Timotheo wa Pili, 4(7) kwamba, Paulo alipomaliza kazi yake akasema, nimepiga vita vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. Nami ninasema hivi, nimepiga vita vizuri kwenye nafasi ya Ubunge, mwendo wa miaka mitano nimeumaliza, (siendi kufa, ingawa Paulo alimaanisha kufa), na hadhi ya Ubunge nimeilinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango na bajeti hii ya fedha tunayoijadili, kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri wamesema, ni mpango wa kimkakati ambao unatupeleka mwishoni kumaliza mpango wetu wa miaka 25 ambao tulikuwa tumeupanga. Tuko kwenye *transition* kuelekea mpango mpya unaofikia 2050, ambao utachukua miaka mingine tena 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaweza kusimama kifua mbele kabisa kuipongeza na kuishukuru sana Serikali yetu kwa kazi kubwa ambayo imeifanya. Kwa namna ambavyo wametekeleza mpango wa miaka mitano, wame-*lay foundation* nzuri sana ambayo tukakwenda vizuri katika mpango unaofuata wa miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu ya miundombinu mikubwa ambayo imekamilika katika Taifa letu, ikiwepo ujenzi wa reli *(SGR)* na umalizaji wa Bwawa lile la Mwalimu Nyerere. Hiyo inatuhakikishia kwamba, tutaendelea kuwa na nishati ya kutosha katika Taifa letu kwa muda mrefu. Hivyo, mipango mingine yote tunayopanga ya uzalishaji itawezekana kwa sababu, tuna nguvu kubwa ya umeme ambao utaendesha sekta zetu zote za uzalishaji na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, miundombinu ya usafirishaji imeimarishwa ikiwemo reli, lakini tunaona katika kila ziwa kuna ujenzi wa meli kubwa ambao unaendelea katika nchi yetu kuonesha kwamba, usafirishaji utaimarika. Tumeona ununuzi wa

ndege zile sita ambazo tumeongeza na utanuzi wa bandari ambao unatuhakikishia kwamba, shughuli za usafirishaji tukizalisha kwenye kilimo na sehemu yoyote zitawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa *foundation* hiyo ambayo mmeiweka na sasa tunaamini kweli, mpango huu wa miaka 25 utawezekana kwa sababu, tayari *foundation* kubwa imejengwa, na mimi sitakuwa nyuma. Kama Mbunge, nilikuwa na wajibu wa aina mbili; kwanza, ni kuwatetea wananchi wangu, mabosi wangu wazito sana, wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini na bila kuwasahau wajumbe wazito walionichagua kwa kura ya maoni, wajumbe wanaotokana na Chama cha Mapinduzi. Hilo lilikuwa ni jukumu langu la kwanza, yale ambayo chama kimenituma kupitia Ilani ya CCM kuyatekeleza katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninapokuwa hapa, ni Bunge la Kitaifa kuangalia mambo yote yanayohusu Taifa letu. Kwenye habari ya Ubunge, wananchi wangu wa Iringa wao ni mashahidi, nimepita kila kata nimewaeleza kwa kufafanua kila kilichofanyika kata kwa kata, lakini yapo mambo makubwa yaliyofanyika ambayo sisi kama Iringa, hatujaachwa. Sisi pia, tumeunganishwa na Taifa hili kwa kutanuliwa uwanja wa ndege, mkubwa. Sasa hivi Iringa ndege zinatua mara tatu kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* wana ndege nyingine kubwa, wananchi wa Iringa wana-*enjoy*. Tulikuwa tunaenda Dar es Salaam kwa shilingi milioni moja, sasa tunaenda kwa shilingi 199,000.00 tu baada ya kutanua Uwanja wetu wa Nduli kwa zaidi ya shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iringa imeunganishwa kwa miundombinu ya barabara. Sisi, kama watu wa Iringa, tunashukuru sana. Ipo Barabara yetu ya Ruaha *National Park* kilometa 104, ambayo inaenda kujengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 140. Barabara ile inaanzia Iringa Mjini mpaka geti la Ruaha, kule *Ruaha National Park.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana tumeletewa Iringa *Bypass* itakayojengwa kwa kilometa 40 na ujenzi wake umeanza. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutuunganisha Iringa na kufanya Iringa kuwa kituo cha utalii kwa maana ya kutuwekea miundombinu ya usafirishaji wa anga, barabara, na pia, kutujengea kituo cha utalii Kusini, pale Kesakilolo. Ni kutuunganisa Iringa na Tanzania, na dunia, na pia, kuongeza kuchechemua uchumi wa wananchi wetu wa Iringa. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamefanyika mengi kwenye elimu. Tumejenga zaidi ya shule tano, tumekarabati shule zetu kongwe za *Iringa Girls* na Lugalo kwa zaidi ya shilingi 1,400,000,000.00. Tumejengewa shule za shilingi milioni 630, karibu tano na tumeimarishiwa Chuo chetu cha Mkwawa, Chuo kikuu, ambapo tumejengewa lami kwa kilometa 3.5 na tumeletewa zaidi ya shilingi bilioni 14, kwa ajili ya mabweni na kujenga *lecture rooms* pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu katika Chuo chetu cha *Roman Catholic (RUCU)*. Tunashukuru mikopo ya elimu ya juu kwa ajili ya chuo chetu cha KKKT ambacho kinaitwa Tumaini *University,* lakini ni *University of* Iringa. Tunashukuru sana, tumefanyiwa mambo mengi kwenye elimu ya msingi kwa kuletewa shule mpya zaidi ya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji Iringa ni 97.8% na umeme Iringa ni zaidi ya 95%. Mamlaka ya Maji Iringa ndiyo mamlaka bora ya pili Afrika kwa kufanya kazi vizuri. Tunawashukuru sana, tumeletewa mbolea kiasi cha kutosha yenye ruzuku, na wananchi wa Iringa wanaendelea kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu yangu ya pili nilikuwa kama Mbunge wa kuliwakilisha Taifa langu. Ninasema vita nimeipiga vizuri, wanaume wa nchi hii nimewatetea, nimesimama nimewasemea umuhimu wa kujenga usawa na kuangalia jinsia zote mbili. Vita nimeipiga vizuri, masuala ya afya ya akili nimeongelea hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kustawisha ubora wa Taifa letu lazima tuendelee kuangalia masuala ya afya ya akili na ninashukuru kwa ahadi ya Serikali, ninaamini kabla hatujamaliza Bunge hili, Baraza la Afya ya Akili nchini litakuwa limeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepambana kuhakikisha kwamba tunasema masuala yale yaliyo kinyume na mila na desturi zetu ikiwemo masuala ya ushoga, ndoa za jinsia moja kupambana nazo na ukatili wa kijinsia. Haya yote tumeyaongea mahali hapa. Zaidi sana tumepata fursa ya kutoa mchango wetu kwa Serikali yetu ambayo ni sikivu na imetusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi, Serikali yetu tunaendelea kuwaombea. Hatukusita kuongelea vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na kuvitia moyo mahali ilipohitajika. Tuliwatia moyo kwamba hatuko tayari kuona nchi yetu inaathiriwa kwa namna yoyote ile kuhakikisha kwamba tunavuruga amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipambana na Mataifa mengine ambayo yalitaka kuleta vurug,u na tuko tayari kuendelea kupambana. Hatutakaa kimya, kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kuwa kisiwa cha amani, na Rais wetu anaendelea kuheshimiwa na anaendelea kupata *comfort* ya kulitumikia Taifa letu akishirikiana na Serikali yake. Hayo tutaendelea kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaiomba Serikali kuhusu mifugo. Moja ya mikakati ya Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa ni kujenga machinjio za kisasa kwenye nchi hii ili mifugo, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Mipango ukurasa wa 21 ile *bullet* 26, kwamba idara atakazoziangalia ni mifugo na uvuvi ili ziendelee kuzalisha zaidi na kuongeza vipaumbele katika uzalishaji wa Serikali. Ninaomba sana, Iringa tulitakiwa kujengewa kiwanda cha nyama. Sasa pale kile kiwanda kimegeuka kimekuwa tena machinjio kwa sababu hakijamaliziwa. Tunaomba kimaliziwe ili kiwe kiwanda na ki-*save* nyanda za juu kusini kwa ajili ya kufanya *packaging* za nyama, kama ilivyokusudiwa kwenye andiko lake, kwamba nyama zitumwe nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Utalii Kihesa – Kilolo nacho kikamilike ili *connection* iwe nzuri. Ndege zipo, barabara inajengwa, lakini kituo cha utalii Kihesa – Kilolo bado hakijakamilika. Watalii wanashuka pale na ndege, hawajui wapi wapate *information* za utalii Nyanda za Juu Kusini. Tunaomba kile kituo kikamilike ili *connection* iwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sekta ya utalii kwa kuwa pia inaongeza sana kwenye pato la Taifa, hasa kwenye fedha za kigeni. Nyanda za Juu Kusini tuwe ni sehemu ya kuchangia utalii wa Taifa hili na kuingizia Taifa letu fedha za kigeni za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu ,baada ya kusema maneno haya ninawashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ninawaomba wananchi wangu wa Iringa, ninaamini wameniona na hawataniacha. Ninawaomba sana Wajumbe waendelee kunikumbuka. Bado nipo, na mambo mengine bado yapo, ninaamini kabisa Mwenyezi Mungu atakusudia, nina kasi zaidi ya nilivyokuwa mwanzo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malembeka anaomba kuwatangazia wageni wake ambao wameingia ndani ya Bunge hili, Machifu kutoka Jimbo la Lindi – Masasi, machifu 25. Karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo wasaidizi wa machifu wanne, machifu wanawake sita kati ya hao Naholela, Mlaponi ni mama yake. Haya mama Malembeka, simama tukuone tena. Hongera sana mama. Ahsante mama, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Rweikiza, wajiandae, *Advocate* Olelekaita, jiandae Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye Bajeti ya Serikali. Ninapenda kuanza kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuigwa mfano. Amevunja rekodi, kama nitakavyoonesha hapa kwenye maelezo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Kitila Mkumbo, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hizo mbili kwa kazi nzuri safi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kagera ninamshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa, Nazir Karamagi kwa kusimamia vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Fatma Mwassa, Mkuu wa Mkoa kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa ilani. Ninamshukuru Mheshimiwa Evarista Babyegeya, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Erasto Sima Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Proskovia Jaka Mwambi, Afisa Tawala wa Wilaya, na Fatina Laay, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya ya Bukoba Vijijini. Tunafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na tunasonga mbele pamoja kwa ushirikiano mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana wananchi wa Bukoba Vijijini, tunafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana kwenye kazi zetu za kila siku za kuleta maendeleo Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Bukoba Oktoba ikifika kura zote ni kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Kama nilivyosema, amevunja rekodi, rekodi ambayo haijawahi kuvunjwa. Ameweka rekodi mpya. Jana mlimsikia Mheshimiwa Byabato, Mbunge pacha wangu wa Bukoba Mjini; sisi tumeshakubaliana na wananchi wetu kwamba, kura zote ni kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze Bukoba pale kwa upande wa sekta ya maji. Mheshimiwa Samia ndani ya miaka minne ameweza kufanikisha kufunga miradi ya maji na yanatoka vizuri katika vijiji 47. Alipoingia alikuta vijiji 14 vina maji, yeye miaka minne ameweza kufunga miradi vijiji 47. 14 vinaendelea na ndani ya muda mfupi kabla mwaka huu haujaisha itakamilika. Kwa hiyo, atafikisha miradi 61 ya vijiji 61 vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye umeme amefunga umeme vijiji vyote 94. Alipoingia alikuta vijiji 41 vina umeme, leo vyote, ameongeza 53 na hivyo vimetimia 94 vina umeme katika miaka minne tu. Ameweza kutusaidia hadi leo tuna vitongoji 281 bado 234 ambavyo havina umeme kati ya vitongoji 515. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya, amekamilisha hospitali ya wilaya. Ameiboresha, amejenga wodi, idara mbalimbali zimeboreshwa, mitambo ipo pale, kama *MRI, CT-Scan* na kadhalika ambayo haikuwepo. Ametujengea vituo vya afya vinne vipya ambavyo vimeanza kazi pale, kama Lukoma, Lubare, Maruku, Kanazi, vyote vinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ametujengea zahanati saba ambazo nazo sasa hivi zinafanya kazi. Ametupatia *ambulance* nzuri, mpya, *Land Cruiser* inafanya kazi vizuri sana. Waganga wapo, wauguzi, vifaatiba, dawa zinapatikana bila shida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye elimu, tumepata sekondari mpya 10, na ni nzuri sana, nyingine zina mpaka maabara tatu, maktaba, na majengo ya kompyuta katika muda huu wa miaka hii minne aliyomaliza. Shule za msingi nzuri mbili pale Kanazi B na nyingine zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata madarasa mengi sana katika Jimbo la Bukoba Vijijini katika muda wake wa miaka minne. Amekarabati shule nyingi na tumepata shule za kidato cha tano na sita *(A-Level),* jumla ya shule sita hazikuwepo. Nimeongea mara nyingi hapa, leo tayari tuna shule za *form five* na *six* sita zinafanya kazi pale Bukoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ametujengea bandari pale Kemondo. Ilikuwepo bandari ndogo ya meli moja, lakini aliyoijenga leo, inaweza kuingiza meli nne, na anajenga sasa hivi *SGR* kuendelea mpaka Mwanza. Ikifika Mwanza, *SGR* tayari kuna meli imeshajengwa pale MV Mwanza, Hapa Kazi Tu. Ikishakamilika hiyo reli ya *SGR* kufika Mwanza, tutanunua *cement* Bukoba kama bei ya Dar es Salaam, ambayo ni shilingi 16,000.00.

Leo ni shilingi 25,000.00 kwa sababu zinakwenda kwa lori, mifuko 400, gharama inakuwa ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishapata treni ya *SGR* na ikafika Mwanza na meli iko tayari na bandari iko pale Kemondo tayari, tutanunua *cement* kama huku mikoa ya Dar es Salaam na majirani. Kwa hiyo, kwa kweli nikisema amevunja rekodi, sitanii, ninasema nikiwa nimedhamiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraja, pale tunajenga madaraja mawili makubwa sana; Daraja la Kalebe na Kyanyabasa. Nimeongea mara nyingi hapa nikipiga kelele kuhusu madaraja haya. Kyanyabasa lina mita 105 na linahudumia kata 18. Leo linajengwa, limefikia 40% au 50%. Ni jambo ambalo kwa kweli hatukutegemea, ni la ajabu, na huyo ndiye Samia Suluhu Hassan, anatupeleka vizuri sana sana. Kwa kweli nikisema amevunja rekodi, narudia si jambo dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kyetema – Kanazi – Ibwera – Katoro ujenzi umeanza kwa kuanza na Daraja la Kalebe ni jambo ambalo nimelisema sana hapa ndani, lakini leo tayari tunapiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amesaidia kupandisha bei ya kahawa. Nimesema hapa kwenye swali, kutoka shilingi 900.00 kwa kilo, leo ni shilingi 5,100.00. Hii ni ajabu kubwa, na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VETA* imekamilika pale Bukoba. Chuo kizuri sana cha *VETA* cha hadhi ya Kimataifa, chuo cha mkoa kipo pale Bukoba. Ametujengea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tawi la Bukoba. Ujenzi umeendelea, uko kwenye 50%. Haya ni mambo makubwa sana, sana, sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo Bukoba hayakuwa na mitandao ya simu, kama Igabiro na mengine, lakini leo wanaongea wakiwa nyumbani kwao. Mtu amelala kitandani anaongea na simu yake, anaongea na mwanaye Dar es Salaam,

na ndugu yake na kadhalika, anatuma fedha na anapokea fedha bila shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Rais Samia anafungua Daraja la Busisi – Kigongo pale Mwanza. Sisi ni wanufaika wakubwa. Kutoka Mwanza mpaka Bukoba ilikuwa saa sita mpaka saba kwa gari, leo ni itakuwa saa nne au tatu kwa sababu siyo mbali, lakini tulikuwa tunakaa pale saa nyingi kusubiri kivuko ambacho ilikuwa ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajengewa uwanja wa ndege wa Kimataifa pale Bukoba Kyabajwa, hayo ni mambo makubwa. Nikisema amevunja rekodi na ninyi, mwelewe kwamba kwa kweli amevunja rekodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapongeza, lakini sisi kazi yetu, mengine ni kushauri na kuiongoza Serikali. Nina ushauri mmoja. Nimesema ameboresha afya, amejenga hospitali, zahanati, na vituo vya afya. Sasa nina ushauri katika eneo hili. Unapokuwa na hospitali ni ya kutibu wagonjwa, lakini tukifungua kila hospitali iwe na kituo cha kupima tiba kinga, kwamba idara hii iwe maalum, chumba kimoja au viwili kwa ajili ya mtu akienda pale apimwe, kuna daktari au kuna wauguzi, anakupima, anajua kwamba huyu anakaribia kuugua ugonjwa huu, wanazuia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumtibu leo mgonjwa aliyeugua kansa ya tezi dume au kansa ya njia ya kizazi ni shilingi milioni 50 mpaka milioni 60, lakini mkizuia huo ugonjwa ni shilingi 200,000.00 au shilingi 300,000.00 tu anakuwa amezuia, tunaokoa fedha za wagonjwa na fedha ya Serikali. Serikali ndiyo mwenye kutoa bima na ndiyo inalipa fedha ya bima. Kwa hiyo, tukipunguza magonjwa hayo kwa kuyazuia kwa kujua tunaokoa fedha ya Serikali na wagonjwa, pia tunaokoa afya za wagonjwa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia kuhusiana na reli nzuri ya kisasa ya *SGR* ambayo sasa hivi inafanya kazi toka Dar es Salaam mpaka Dodoma. Pale Pugu paongezwe kama kituo cha

Dar es Salaam. Inasimama ile treni ya kawaida, lakini *express* haisimami pale. Dar es Salaam ina vituo viwili vya *express* Dar es Salaam yenyewe pale *Station,* na Pugu hata kama ni *express* ile pale Pugu isimame.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wote ambao wanatoka Dar es Salaam Kaskazini Mbezi Luis, Mbezi Beach, Kunduchi hata Mikocheni, Sinza, Tegeta watapata faida pale. Badala ya kwenda pale *station* ambako kunakuwa na foleni kubwa sana, pale Pugu iwe ni kituo cha pili cha Dar es Salaam hasa kwa treni ya *express. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na shida kwenye suala la ajira ya vijana. Suala la ajira ya vijana nilikuwa nina tatizo kubwa, lakini nimesoma Ilani ya CCM ya mwaka huu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia, dakika moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma Ilani ya CCM ya Mwaka 2025, nimeridhika kwamba CCM imejipanga kwa ajili ya kutatua tatizo hili la vijana kupata ajira. Kwa hiyo, sina shida na hilo, shida imekwisha. Nina hakika kwamba tatizo hili litatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Advocate* Edward Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtenga, na Mheshimiwa Subira.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu, ametulinda miaka mitano yote hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia kwa sababu Bajeti Kuu ya Serikali tunayoihitimisha ni hitimisho la awamu ya kwanza ya Meshimiwa Dkt. Samia. Ametekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kishindo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Prof. Kitila Mkumbo, Dkt. Mwigulu Nchemba, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wote wawili wa Fedha, Mipango na Uwekezaji; rafiki yangu wa Kamati Kuu shikamoo; Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu, na wataalam kwa hotuba hizi mbili za hali ya uchumi na Bajeti Kuu ya Serikali. Tunaipongeza pia Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia kwa miaka minne ya uongozi wake na utekelezaji wa Ilani wa Chama cha Mapinduzi 2025. Ilani hii imetekelezwa kwa viwango vya juu sana na kwa umahiri mkubwa sana. Kishindo cha Mheshimiwa Dkt. Samia kupitia miradi ya maendeleo kimesikika kwenye majimbo yote Tanzania na kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ya maendeleo imetujengea Waheshimiwa Wabunge heshima kubwa sana kwenye majimbo yetu. Imeleta kigugumizi kikubwa sana kwa wale wanaotamani majimbo haya kwa sababu wananchi wameona miradi ya maendeleo ikitekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kiteto tuna miradi ya zaidi ya shilingi bilioni 160. Shule za sekondari, vituo vya afya, shule za msingi takribani 20, maji, miradi kila mahali. Kwa kweli hii imekijengea taswira na heshima kubwa Chama chetu cha Mapinduzi kwa wananchi wa Tanzania; na ninadhani ndani ya miaka mitano tumejenga uhalali wa kuliongoza Taifa hili kwa kipindi kingine tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawashukuru sana wananchi wangu wa Kiteto kwa ushirikiano mkubwa sana walionipa na kwa ari yao ya kupenda maendeleo.

Ninawashukuru na viongozi wa mkoa, Mheshimiwa *RC,* Mwenyekiti wa CCM na viongozi wote; *DC* na Mkurugenzi wa Wilaya ya Kiteto na Wataalam wote kwa ushirikiano walionipa kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti Kuu hii ya Serikali ina sifa takribani tatu kubwa. Kwanza, inahitimisha dira ya maendeleo ya Taifa ya miaka ya 2025. Tunahitimisha na Bajeti hii Kuu ya Serikali. Pili, inahitimisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025; na ninadhani huu utekelezaji wa ilani unaoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia imetujengea heshima kubwa sana na inatupa fursa kubwa ya kuendelea kuomba ridhaa ya Watanzania kwa kipindi kingine kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumza habari ya ajira, tumekwenda zaidi ya tulivyoahidi kwenye ilani. Tuliahidi ajira milioni nane, lakini Bajeti Kuu ya Serikali hapa ajira imekuwa zaidi ya milioni nane. Kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tulisema tutapeleka umeme vijijini. Tumemaliza na tunakwenda kwenye vitongoji sasa. Hatukuwa na vitongoji kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunavyosema, hatumdai Mheshimiwa Dkt. Samia tunamaanisha. Ni utekelezaji wa ilani na mkataba tulioandika na Watanzania, amemaliza kwa kishindo kikubwa sana. Haimaanishi kwamba tumemaliza matatizo yote, hapana, ndiyo maana tumeandika ilani nyingine ya miaka mingine mitano ijayo. Maendeleo ni safari, lakini tulichoahidi kupitia ilani hii Mheshimiwa Dkt. Samia ametekeleza kwa viwango vya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii vilevile, inahitisha safari ya miaka mitano ya Bunge la Kumi na Mbili. Kwa hiyo, ni bajeti kuu ambayo ina sifa hizo. Bajeti Kuu ya 2025/2026, ili kuweza kupima uzuri wa utekelezaji wa bajeti ama mipango yenyewe ni lazima iwe na sifa zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, lazima iseme ina kitu kinaitwa *fiscal responsibility,* ama nakisi inayoweza kudhibitika ambayo haileti deni ambalo litatikisa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hotuba hii utaona mipango, deni letu himilivu, lakini lingine ni lazima tuone ukuaji wa uchumi na uhimilivu *(economic growth na stability)* na zote ziko kwenye bajeti hii. Sifa ya bajeti tukipata misukosuko, je, tunaweza tukapambana nayo? Ndiyo sifa ya bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata majanga mengi hapa, kwa mfano, Hanang kule hakuna mtu aliyetegemea, lakini kama kuna jambo ambalo Serikali imefanya kwa viwango vya juu sana na kila wakati ninawaambia, ambayo inastahili kurekodiwa, namna bora ya kupambana na majanga ni namna Serikali ilivyopambana na janga la Hanang' kule. Kwa hiyo, bajeti yetu lazima iweze kupambana na mabadiliko ya uchumi na sera za Kitaifa. Ukisoma bajeti hii, utakuta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa ya bajeti ni lazima iwe na usawa wa kijamii *(social security)* je, inapambana na umaskini? Inapambana na ujinga na maradhi? Hospitali tunazojenga na vituo vya afya tunaendelea, tuko kwenye safari ya kupambana na maradhi. Ujinga: shule tunazojenga na vyuo na miradi iliyoko hapa, lakini tunakuza uchumi tunapambana na umaskini. Ukisoma bajeti hii, utakutana na vitu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni uwazi kwenye usimamizi wa matumizi ya Serikali. Ukisoma hotuba hii, utakutana na mipango. Kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali, kazi ya CAG kila wakati ni kufuatilia namna ya kuweka nidhamu na kuongeza *transparency* na *accountability,* na zote ziko hapa. Sifa nyingine ya bajeti inatoa vipaumbele kwa miradi ambayo inaleta pesa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukisoma vilevile bajeti hii utaona kila kitu. Vilevile, bajeti lazima ioneshe vyanzo vya mapato, na vyanzo vyetu ni kodi. Ni lazima tulipe kodi. Kwa hiyo, mapato mengi yanatoka *TRA,* mapato yasiyo ya kodi ndiyo

vyanzo vingine, mapato kutoka Serikali za Mitaa, mikopo ya nje na ya ndani, pamoja na misaada. Kwa hiyo, hoja hapa siyo mikopo, kila mtu anakopa, hata sisi wenyewe tunakopana huko mtaani. Tatizo, tunatumiaje mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunachukua leo hii mkopo kama ule wa UVIKO – 19 na kupeleka miradi katika majimbo yote Tanzania, nani ana-*questions* kuhusu mikopo? Kama tunachukua leo tunajenga Daraja la Busisi ama Bwawa la Mwalimu Nyerere ama *SGR* ambaye kila mtu anapanda na anafurahia huduma hiyo. Ama kufanya bandari yetu ambayo ndiyo inaleta asilimia kubwa, karibu 40% ya mapato ya *TRA;* kama tunafanya hivyo na tunaendeleza uchumi wetu, nani analeta hoja za kukopa hapa? Sisi ni nchi maskini, mikopo ni chanzo kikuu na ni muhimu sana. Tukiongeza mapato yetu, na siku tukaondokana na hilo, hakuna mtu atataka kukopa… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *advocate,* malizia…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Ninadhani bajeti yetu imekidhi viwango vyote vya Kimataifa na sifa kuu za bajeti. Kwa hiyo, niongee na Watanzania wenzangu kwamba mwaka huu wa uchaguzi tumchague Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kishindo kikubwa sana. Zawadi pekee ni kushiriki kwenye uchaguzi huu mwaka huu na mimi ninawatakia na Wabunge kila la heri Mwenyezi Mungu awabariki. Ahsanteni sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, jiandae Mheshimiwa Mgalu, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakushukuru nami kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Bajeti Kuu iliyokuwepo mbele yetu, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku ya leo na takribani miaka yote mitano tukiwa

humu Bungeni tukitekeleza majukumu tuliyopewa na wananchi ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ni Rais wa pekee Afrika. Kwa muda mfupi ameonesha uimara wake na uthubutu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwahudumia Watanzania, kwa kutuletea maendeleo ambayo yametukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Mawaziri wote wawili ambao leo tunajadili bajeti zao. Kaka yangu, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo niseme ninamshukuru sana, sana, sana kwa sababu amefika mahali ameonesha sasa alichomwagiza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufungua Mtwara, amelipokea, na sisi tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Rais kwa ujenzi wa bandari ya kisasa ambayo iligharimu zaidi ya shilingi bilioni 157 ambapo sasa meli ya aina yoyote ile inafunga pale na shughuli nyingine za kijamii zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiingia kwenye suala la afya, tunayo hospitali yetu ya kanda ambayo ilisimama kwa muda mrefu sana, lakini alivyoingia Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliweza kuiwezesha hospitali hii na sasa imekuwa ni hospitali ya mfano kwenye kanda ya kusini. Watu wa Msumbiji na maeneo mengine wanapata tiba pale. Tunamshukuru sana Rais na tunajivunia Wanamtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu wananchi wa Mtwara walikuwa wanatembea zaidi kilometa 400, 500 kwenda kutafuta huduma ambazo zinaweza kupatikana Muhimbili na maeneo mengine. Kwenye hili tunamshukuru sana Mheshimiwa Rasi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, wakati tunaingia mwaka 2020 tulikuwa tuna shida ya maji Mtwara. Maji yetu

yalikuwa yakitoka kwenye bomba, unaona ni maji ya njano kama jezi ya *Young African,* lakini Mheshimiwa Rais aliweza kutupatia fedha za kujenga chujio la kisasa zaidi ya shilingi bilioni 3.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu hakuishia hapo tu, akatuletea fedha tena shilingi bilioni 29 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu na kuweka mabomba ya kisasa kwa sababu bomba zote ambazo zilikuwepo ni bomba ambazo ziliwekwa na mkoloni na bomba zile zilikuwa za chuma. Haya yote Rais ameona kwamba kuna haja ya kuwawezesha wananchi wa Jimbo la Mtwara wapate maji yaliyokuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo mradi huo tu, ametujengea tenki kubwa pale *airport* la zaidi ya shilingi milioni 500, na tenki hilo limeanza kufanya kazi maeneo yote ya pembezoni zaidi ya kata kama nne, tayari maji yameshaanza kupelekwa, na wananchi wanakunywa maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninamshukuru tena Mheshimiwa Rais, tulikuwa tuna mgogoro mkubwa sana baina ya wananchi na tajiri mmoja ambaye sasa hivi ni marehemu. Eneo lile Mahakama iliamuru kwamba nyumba zile zote zivunjwe, lakini baada ya hapo tukarudi tena Mahakamani, tukatumia diplomasia, na Rais akaweza kutusaidia nyumba zile zimebaki, wananchi wale wamebaki, na sasa hivi wanaendelea kupewa hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Rais wa pekee kufika mahali akatambua kwamba kuna wananchi ambao wanapata shida na wanatakiwa kusaidiwa. Vilevile, katika eneo ninalozungumza la visima vyetu vya maji, Mtawanya, miaka hiyo wakati panatengenezwa visima hivi vya maji wananchi walitoa ardhi zao takribani miaka 30 iliyopita, lakini walikuwa hawajalipwa fidia. Nilipiga kelele Bungeni na Mheshimiwa Rais alisikia hilo, akatupatia fidia, pesa zaidi ya shilingi milioni 770. Nani kama Mama Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema yale yanayosemwa kwamba sisi hatuna deni, yaani tunachelewa tuone lini

tunakwenda kumpigia kura Rais huyu wa mfano ili Watanzania na maeneo mengine wajue kabisa kwamba wananchi wa Mtwara Mjini wameridhika na huduma za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hospitali zetu mbili, tuna hospitali ile ya kanda, na tuna hospitali ya rufaa. Hospitali hizi zote zilikuwa hatuna vifaatiba, lakini ukienda hospitali za kanda ya kanda pale utakuta kuna ma-*CT scan,* na kuna *MRI.* Mashine zote ambazo ziko Muhimbili unazikuta pale Hospitali ya Kanda Mtwara. Pia ukija kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, huduma zote zinazopatikana kwenye hospitali ya kanda zinapatikana pale. Hongera sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo letu la Mtwara Mjini tuna takribani kata zaidi ya 11, hazina shule za sekondari, lakini Rais, Dkt. Samia ametuwezesha ndani ya miaka hii mitano kutupatia shule za sekondari tatu za kisasa, za mfano ambazo zina maabara na mambo ya sayansi yameanza mle, na vijana wameshaanza kuji-*tune* kwa ajili ya kusomea sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, tumepata shule za msingi mbili za kisasa. Tumepata pale Chihiko Kata ya Mtawanya lakini tumepata shule nyingine pale Ufukoni. Shule hizi ni nzuri na ni shule za mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo wananchi wa Mtwara wanamwombea Rais wao awe na maisha marefu ni kutukubalia kutujengea Daraja la Mozambique na Tanzania pale Mto wa Kilambo. Hili ninasema, katika kelele zote tulizokuwa tunazisema hapa Bungeni kuhusu ujengwaji wa daraja lile Mheshimiwa Rais amelipokea na tayari liko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapozungumza, wananchi wa Mtwara wanamsubiri Rais wao sasa wampokee kwa shangwe na sherehe jinsi yeye anavyofika mahali akasema kwamba Mtwara ataifungua. Neno la Rais analosema ataifungua Mtwara

limeanza kuonekana siyo kwenye daraja tu. Leo katika *airport* ile tunajengewa sasa jengo la abiria la kisasa na ameshaleta fedha zaidi ya shilingi bilioni 63 tunakwenda kujenga Mtwara *International. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuzungumzia suala la mazao. Mtwara ni eneo ambalo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malizia.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara ni eneo ambalo kilimo chetu ni cha korosho, lakini hatujawahi kuuza korosho kilo shilingi 4,200.00 na kuendelea. Rais huyu wa sasa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametuwezesha kupata mbolea za kisasa na wakulima wakapata mbolea, na sasa korosho imekuwa ni hitajio kubwa, lakini hata hivyo wananchi wa Mtwara wameanza kuwa matajiri kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu, halafu Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, na Mheshimiwa Ighondo wajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi ya leo kutoa mchango wangu kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2025/2026. Nami niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ametuwezesha kulitumikia Bunge hili la Kumi na Mbili na hatimaye tunaelekea ukingoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi ninamshukuru sana kwa afya njema kwa viongozi wetu na kwa sisi sote, na leo michango ya Bajeti ya Serikali ambapo mimi nimechangia karibu kila mwaka, na leo ni mchango wangu wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, nikushukuru na wewe Naibu Spika kwa namna ambavyo mmetuwezesha sisi Kamati yetu ya Bajeti tangu mlipotuteua kwa miaka mitano mfululizo, tumefanya kazi hiyo kwa uadilifu, weledi na kujitoa. Hapa niipongeze sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kipindi chote cha miaka mitano ya kutumikia hii Kamati ya Bajeti, kwa kweli wametoa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Serikali sikivu pale ambapo tulikuwa tunabishana ilikuwa ikitafakari, ikiona hoja ya msingi na ikikubali mapendekezo yetu, na kwa kweli tumeenda vizuri mpaka tutakapohitimisha tutapopitia hii *Finance Bill. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombee dua viongozi wetu wote, Spika na wewe Naibu Spika katika mchakato mnaoendea na wao Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Prof. Kitila na Manaibu wote kwa namna ambavyo wamefanya kazi, Mwenyezi Mungu awawezeshe kuwarejesha, pia na Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina faraja kubwa ninapohitimisha kuchangia bajeti hii ya mwaka huu, kwa sababu kama nilivyosema, nimechangia bajeti zote, lakini faraja yangu ni kuona ninachangia kitu ambacho kinaleta manufaa kwa Taifa. Tunachangia bajeti ambazo wanafikia malengo, wanakusanya, na fedha zinafikia kwenye miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi kwamba bajeti wakati tunaanza awamu hii ya sita kutoka makusanyo ya zaidi ya shilingi trilioni 25 mpaka sasa tunapohitimisha nyongeza ya makusanyo ya mwaka huu, matarajio ya kufika trilioni 30 na kuvuka malengo kwa mara ya kwanza kulingana na kiasi ambacho walikadiriwa kwenye mapato ya ndani, kwa hiyo, hicho ni kipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo kingine kwa Serikali hii kufanya vizuri ni kwa matumizi ya maendeleo ya hasa kwenye mapato ya ndani, kutoka shilingi trilioni tisa mwaka 2021 mpaka shilingi trilioni 12 mwaka huu 2024/2025 unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, ukurasa wa 22 mpaka 23 ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupambana na maadui watatu: ujinga, umasikini na maradhi kupitia kazi mbalimbali alizozifanya katika kuingoza hii Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa nini Mheshimiwa ninasema hivyo? Kwanza, sisi katika Mkoa wa Pwani tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani kwa bajeti zote mpaka Machi, 2025 tumepokea kiasi cha shilingi trilioni 1.35 fedha za kwenye maendeleo, lakini pia kugharamia shughuli mbalimbali za Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mapambano dhidi ya ujinga, tunamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na jitihada zote za Kitaifa, na jana tumeona akizindua shule ya amali kuwakilisha shule 103. Kwa Mkoa wa Pwani, tunamshukuru kwa kiasi cha shilingi bilioni 83 alizotuletea kwa ajili ya miundombinu ya elimu, lakini pia kwa ajili ya elimu bure ambayo amekuwa akiiendeleza mpaka kufikia kidato cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujenzi wa shule mpya, ujenzi wa shule ya wavulana, ujenzi wa shule ya wasichana, ujenzi wa shule nne za amali, na ujenzi wa vyuo zote, tumepata na tunaamini kwa kupitia miundombinu mipya na kwa mara ya kwanza tumepokea fedha nyingi kwenye sekta hii. Ni wazi ujinga katika mkoa wetu, Mheshimiwa Rais amepambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, katika mapambano ya umaskini ndani ya mkoa wa wetu, tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa uboreshaji wa miundombinu ya barabara, na madaraja kiasi cha shilingi bilioni 92 kwa ajili ya barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ujenzi wa madaraja, hapa ninaomba niliseme, Daraja la Wami Mkoa wetu wa Pwani, Daraja la Mbuchi visiwani *delta,* Daraja la Mbwera, Daraja la Mbambe pamoja na Daraja la Muhoro yamesaidia sana kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao, kuwezesha kufunga kwa

mawasiliano na kuwezesha shughuli za kiuchumi kuchangamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, katika kupambana na umaskini, sekta ya nishati kukamilika kwa Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere wa shilingi trilioni sita, unajengwa ndani ya mkoa wetu wa Pwani, kukamilika kwa *substation* ya Chalinze, na kukamilika kwa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rufiji mpaka Chalinze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye sekta ya viwanda, ongezeko la viwanda 135 ndani ya mkoa wetu wa Pwani, ambao umezalisha ajira nyingi; pia, ongezeko la ruzuku ya mbolea kwa wakulima wetu wa korosho pamoja na bei nzuri ya korosho na mazao ya ufuta, ninaamini ni kupambana na umaskini. Amekuwa Rais ambaye amefanya hayo kwa kiwango zaidi kuliko wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwenye kupambana na maradhi, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa zaidi ya shilingi bilioni 28 alizopatia Mkoa wetu wa Pwani. Kipekee kwa Hospitali yetu ya Rufaa ya Tumbi kwa kuhakikisha hospitali ile kwa mara ya kwanza ina *CT-Scan,* wodi za *ICU* na *emergency*. Pia, kutujengea vitu vya afya zaidi ya 19, kutukarabatia hospitali za wilaya, na kutujengea zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee utaratibu wa kusafirisha wajawazito M-Mama kwenye maeneo ya *delta* umewezesha kupunguza vifo vya akina mama, na ni wazi kwamba mkakati huu umepambana na maradhi ya ndani ya Mkoa wetu wa Pwani na kutuwezesha kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima hilo la nishati, ninapenda kutoa shukurani za dhati kwa namna ambavyo wametuwezesha eneo la visiwani. Ilikuwa haitarajiwi kupata umeme wa gridi ya Taifa, lakini leo ukienda Kibiti, Kata za Mbuchi, na Kihongoroni, huko kote kuna umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru ilani inayoendelea sasa hivi na kwa kweli Mheshimiwa Rais hana deni kwa kuleta Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Bagamoyo. Hata hivyo, ahadi ya kulipa fidia ni kilio cha miaka mingi tangu 2015 wakazi wa Kata ya Zinga maeneo ya Mlingotini, Pande, wanaenda leo kupata ahueni ya kulipwa fidia na tarehe 26 Serikali itakuwa Wilayani Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambayo tulikuwa tunaitarajia muda mrefu pia utaongeza shughuli za uvuvi katika Wilaya yetu ya Bagamoyo. Kwa mara ya kwanza pia tumeshuhudia kilio cha kulipwa fidia cha Barabara ya Tanga – Pangani – Mkange inayoelekea Makurunge fidia imelipwa mwaka huu 2025. Ilikuwa kilio cha muda mrefu lakini Serikali imelipa fidia Barabara ya *TAMCO* kwenda Mapinga ambayo ilikuwa kilio cha muda mrefu. Hizo zote ni jitihada za kupunguza umaskini wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kweli Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hana deni amefanya kazi nzuri na inaoekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie pia kwa kuwashukuru UWT wa Mkoa wa Pwani kwa kunipatia fursa ya kuwa Mbunge wa vipindi vitatu kwa Chama Cha Mapinduzi kwa uongozi wa juu. Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu, Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa wagombea ndani ya Chama Cha Mapinduzi na kwa viongozi wangu ma-*boss* wangu wa UWT Taifa, Mama Mary Chatanda, Mama Zainab Shomari na Katibu Mkuu Mama Suzan Kunambi kwa kazi nzuri ya kutembelea miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposimama hapa tumetoka kwenye ziara Mkoa wa Pwani, tumetembelea miradi zaidi ya 131 yenye thamani ya bilioni 359; tumefanya mikutano ya hadhara 77. Yote hayo ni mazingira yaliyowekwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufanya Vyama vya Siasa vifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hakuna wa kulinganishwa naye. Tumefanya kazi ya kibunge kwa wepesi. Tunamshukuru kwa majiko ya gesi 200 aliyotupatia. Tunamshukuru kwa mashuka 100 kila Mbunge Mwanamke aliyepatiwa tumepeleka katika maeneo yetu. Hakuna wakati kazi ya kibunge imekuwa rahisi kama Bunge hili la Kumi na Mbili, unapata ziara unafanya, hakuna maeneo hukosi la kusema. Kwa hiyo, ninataka kusema Mkoa wa Pwani tumejipanga kumpatia kura za kishindo Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hana deni nchi nzima na hana deni ndani ya Mkoa wetu wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Hongera kwa Wizara ya Fedha na taasisi zote waliofanya kazi hii nzuri. Hongera Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kuanza kazi vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, wajiandae Mheshimiwa Ighondo, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Nimshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote aliyetuwezesha kipindi cha miaka mitano kuwatumikia wananchi na hususan Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na Wilaya ya Muleba. Ninaishukuru familia yangu kwa kuniwezesha, kunilinda na kuniombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano au hii Awamu ya Sita. Kwetu Muleba tunasema tunaunga mkono bajeti hii na tunamuunga mkono Rais wetu kwa kazi kubwa alizozifanya kwa kipindi cha Awamu yake ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenye macho hawaambiwi angalia na mambo yote yaliyofanyika kwa kipindi cha miaka mitano hatuhitaji kuyatangaza, yanajitangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapoongea Muleba tunafanya sherehe kubwa. Kahawa walikuma walikuwa wanauza shilingi 5,000, jana nimepokea taarifa kahawa imeapanda kutoka shilingi 5,000 imekwenda 11,755 kwa bei ya *Robusta*, maganda wanauza kwa shilingi 5,500. *Arabica* inakwenda 11,500 kahawa safi na shilingi 5,500 kwa *Arabica* maganda. Hii ni kazi ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Ninawashukuru Waziri Mkuu alifanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata bei nzuri na ninamshukuru Rais wetu kwa sababu ndiye aliyemtuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Mawaziri kwa bajeti hii nzuri waliyotuwasilishia hapa Bungeni**.** Binafsi nimshukuru Mheshimiwa Chande kwa kazi kubwa anayoifanya, viongozi wote wa Wizara na Makatibu Wakuu. Kusema kweli kama Mbunge wa Jimbo la Muleba Kusini ninasema na juzi tumepita tumekubalina kwa Muleba tunakwenda kuwa namba moja kwa kura za Rais Oktoba. Wanaotaka kushindana waje wajifunze kwetu na tunayo sababu ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninamshukuru Rais anazindua Daraja la Busisi, lakini kwetu pale Muleba tuna Daraja la Mto Ngono na Daraja la Kamishango. Kusema kweli ni mfupa ulioshindikana miaka nenda rudi, lakini tunavyoongea Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha shilingi 12,500,000,000 tunajenga lile daraja ambalo lilikuwa ni shida kubwa kwa Wafanyabiashara wa Wilaya ya Muleba kwa sababu maeneo yote ya Nshamba na Mgongo wafanyabiashara wanaoleta magari makubwa walikuwa wanalazimika kushusha mizigo kupakia kwenye magari madogo, ili wapite kwenye daraja lililokuwepo, lakini Mama Samia amesema hayo sasa basi, tunamshukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, inakwenda kuchangamsha uchumi kwa sababu bidhaa zilikuwa zinauzwa kwa bei kubwa kwa sababu ya gharama kubwa ya usafirishaji. Vilevile, kana kwamba hilo halitoshi ninakushukuru nimesema Mheshimiwa Chande alitusaidia sasa Hospitali ya Wilaya ya Muleba

Makandarasi wapo *site*. Majengo yanapanda kwa kasi na Wanamuleba wanasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamesema hapa sisi kwetu Muleba tumejenga shule mpya 16 ambazo zimepunguza umbali wa watoto wetu kwenda na kurudi shuleni. Shule zenyewe ni za vigae zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa ninaongea na mama mmoja akaniambia alikuwa na biashara yke ya kuuza viatu vya wanafunzi akasema biashara yake imekufa kwa sababu Mama Samia amejenga shule karibu na wanafunzi, hawasafiri umbali mrefu. Kwa hiyo, viatu walivyokuwa wanatumia havichaniki kwa haraka kwa sababu wanasafiri umbali mfupi. Hii ni kuchangamsha uchumi. Yule mama nilimwambia pole, lakini hongera hiyo ndiyo kazi ya Chama Cha Mapinduzi na ndiyo kazi waliyotutuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo kwa Wilaya ya Muleba hatuna jambo, hatuna neno lolote. Kazi yetu ni kwenda kujaza kura Oktoba wameshakubalina ni kwenda ku-*tick* tu hatuna jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu; 2020 kuna maeneo ambayo yalikuwa hayafikiki. Kwangu pale kwenda Burigi ninadhani wananchi wa Burigi wananisikia. Wakati ninakwenda kuomba kura ilibidi nitumie pikipiki, lakini juzi nilienda pale nimeshangaa mpaka daladala zinafika na zinalala kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyofanyika ni kubwa na ndio maana ninawaomba Wanamuleba tutoe turudishe shukrani yetu ifikapo Oktoba na kazi lazima iendelee na Muleba inakwenda kuwakawaka kama ambavyo wilaya nyingine zimefanya. Hayo yaliyofanyika Muleba yamefanyika wilaya zote na hii ni kazi ya Rais wa Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana niwaombe Wanamuleba, Mbunge wanaye yupo anarudi hakuna *propaganda* na mbambamba, kazi tumeifanya na

aliyetuwezesha ndiy huyo tunakwenda kumrudisha. Kwa hiyo, yaliyofanyika awamu hii ndiyo yale yatakayofanyika awamu ijayo. Tuendelee kumwomba Mungu atupatie uzima, ili tuendelee kutumikia wananchi wetu. Kazi imefanyika na itaendelea kufanyika na ndiyo hiyo falsafa ya Mama, kazi iendelee na kweli itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yapo mbele ila kwenye hili nishauri mambo machache. Kwenye bajeti iliyowasilishwa Mheshimiwa Waziri ameongelea kwenye *para* 15 ya hotuba yake Sheria ya Msajili wa Hazina ameongelea kubadilisha vipengele viwili, kipengele cha 8A na 8F. Ninaomba hiyo sheria badala ya kubadilisha hicho kipengele pekee, tukaifanyie marejeo sheria nzima kwa sababu tunataka fedha na Msajili wa Hazina…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Kikoyo, malizia.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ighondo, jiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nami fursa, ili niweze kusema maneno machache ya muhimu ya ku-*wind up* hotuba zangu tano za bajeti hii, ya tano tangu mimi nikiwa Mbunge mwakilishi wa Jimbo la Ilongero tangu waliponipatia kura mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukuombea wewe jirani yangu mtaani hapa. Ninakuombea afya na tarehe 28 uende ukachukue fomu na tarehe 2 Mwezi wa Nane ushinde kwa kishindo. Tuna imani na wewe pia ninawaombea na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, niwaombee afya na

kila la kheri katika michakato hii inayoanza ili na wao waende wakarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu ya kazi nzuri ambayo imefanywa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan katika maeneo yetu. Pia unafahamu timu huwa ina *first eleven;* Mheshimiwa Rais ameshatengeneza timu yake *first eleven* analo Baraza lake la Mawaziri ni zuri, anao Wabunge wake hawa wazuri. Kwa hiyo, hakuna haja ya kufanya vurugu kuwaondoa hawa Wabunge, wote watarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende niseme kwamba nimesoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeipitia maeneo mengi. Ninampongeza Waziri kwa hotuba yake na Mheshimiwa Kitila pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi yao nzuri wanayoifanya, kimsingi wanatusikiliza. Hawa sisi tunaitana *comrades* huwa ni watu ambao ni wasikivu na wanyenyekevu, tunaongea nao. Hakuna tofauti unapoongea na Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri ni kama unaongea na Mbunge mwenzako. Kwa hiyo, ninawapongeza na waendelee na utu na utendaji huo wa unyenyekevu katika kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina michango yangu kwenye mambo machache ninataka nizungumzie kwa kulingana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nitakwenda kuzungumza kwenye eneo la *production sectors* (sekta za uzalishaji) pia miundombinu ya usafiri na usafirishaji na maeneo ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza na haya nizungumze kidogo kuhusu tathmini yangu ya hii bajeti; ni kwamba tunapokwenda kuhitimisha Bunge hili la mwisho tunapoelekea kwenye uchaguzi, mimi kwa upande wa Jimbo langu la Singida Kaskazini tunakwenda kusema ndiyo tarehe 24 kwenye hii bajeti kwa sabbu kubwa zifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwenye maeneo ya huduma za kijamiii, eneo la afya jimbo letu limepata vituo vya afya, hospitali ya wilaya na zahanati. Kwa hiyo, kwenye eneo la afya lazima tukaseme ndiyo ili hizi huduma ziendelee kuboreshwa.

Hapa tunapozungumza tunayo milioni 250 haijaanza kutumika ipo kwenye akaunti pale Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kinyagigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tunayo pia hapo hapo fedha zinaendelea, ujenzi unaendelea pale kwenye Kituo cha Afya Ngimu shilingi milioni 686. Sasa hivi nina sababu gani ya kuja kusema *no* kwenye hii bajeti? Sisi wana Singida Kaskazini tumeheshimishwa sana na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, bado tunataka tuendelee kumuunga mkono na hizi fedha ziendelee kuja ili wananchi wetu waendele kupata huduma. Huko kwenye afya leo tuna madaktari. Leo Ilongero tuna Madaktari Bingwa Ilongero kule ninadhani Waziri anaifahamu Singida. Tuna Madaktari Bingwa kule Ilongero wanafanya na upasuaji kwenye hospitali zetu, vituo vya afya pamoja na wilaya. Sasa kwa nini asiseme ndiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo pia shule nyingi ambazo zimeota za msingi na sekondari kwenye maeneo yetu; Kiomboi Sekondari, Sekoutoure, Msange Sekondari, Msimii Primary, Minyaa Primary na zinaota kama uyoga. Unaona unaanza msingi, shule inaenda moja kwa moja kwenye kukamilika. Sasa ni lazima tuseme ndiyo, ili wananchi wetu waendelee kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumza kwenye hizi sekta za uzalishaji ambazo nimeona hata Mheshimiwa Waziri amezizungumza kwenye hotuba. Nchi yetu inahitaji kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Tunahitaji kwenda kwenye uchumi wa mtu mmoja mmoja. Tuimarishe uchumi wa mtu mmoja mmoja na 90% ya wananchi wetu wapo kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nimeona Mheshimiwa Waziri ametupatia hata takwimu kwamba sekta hizi zimechangia kwa 4.05% kwenye uchumi wa nchi yetu. Sasa ni lazima hizi sekta ziendelee kuimarishwa, ili tuweze kuzalisha ipasavyo, hizi ndiyo zitakazolisha viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuondoke kwenye kuagiza *raw materials* nje ya nchi kuja kuhudumia viwanda nchini. Sisi hapa tuagize *raw materials* kutoka nje zije zihudumie viwanda vyetu. Siyo sisi kuchukua mahindi kupeleka Kenya, kuchukua samaki kupeleka Ulaya, kuchukua pamba kupeka Ulaya. Inatakiwa sisi tuzalishe halafu viwanda vyetu humu vihudumie wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi zitaongeza ajira hata zile nyingine ukiacha zile za moja kwa moja kwenye kilimo, hata *informal* zile ambazo inaenda kutokana na *production* inayofanywa na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa na miundombinu mizuri ya barabara, reli kama unavyoona sasa hivi *SGR* na ninaomba sana hii *SGR* ikamilike iende mpaka kule kwenye mpaka wa nchi yetu. Iende mpaka kule Isaka na Kigoma ili mazao yanayozalishwa kule yaje kwenye eneo lenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapozungumza eneo la miundombinu ninagusa pia kwenye eneo la jimbo langu. Tuna barabara za muhimu ambazo zinahitaji kuboreshwa zaidi, kwa sababu sisi kule tunalima na kufuga. Sasa ile mifugo tunayosema twende kwenye kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye viwanda au kwenye masoko, ni lazima tuwe na miundombinu mizuri ya barabara, ili ziweze kusafirishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ninasema ile barabara yetu ya kutoka pale Igauli kwenda Ilongero kwenye Makao Makuu ya halmashauri kilometa 11.5, ikamilike kwa wakati Iende mpaka Haydom ikamilie kwa wakati, ili tuunganishe Mkoa wa Simiyu, Manyara na Sindiga waache kuzunguka kutumia ile barabara ya mbali inayotoka Mwanza, ili kuwarahisishia wananchi kuwapunguzia gharama pamoja na usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo kwenye barabara pia tunayo madaraja makubwa. Leo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kipenzi chetu anazindua Daraja la muhimu sana la

kilomita tatu lile la Kigongo – Busisi. Haya ni mageuzi makubwa sana ya uchumi wa nchi yetu na ndio ambayo tulikuwa tunasema lazima yafanyike.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo malizia kwa mchango mzuri, malizia.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, pia ninasema Serikali yetu lazima tuhakikishe tunapeleka nguvu za kutosha, tunaweka vipaumbele kwenye sekta za uzalishaji, ili ziweze kulisha viwanda vyetu na sisi tuweze kuajiri jamiii yetu ambayo kwa kiwango kikubwa ipo huko chini kwenye maeneo ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Pia, umeme uendelee kufika mpaka kwenye vitongoji kama alivyosema Mheshimiwa Rais wetu juzi akiwa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kaijage na Mheshimiwa Atupele Mwakibete.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Bajeti Kuu. Hotuba yangu la leo itajikita zaidi kwenye kushukuru na kupongeza na hapa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kudumu kwenye nyumba hii miaka 10 leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee vilevile kumpongeza na kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyoisimamia Ilani cha Chama Cha Mapinduzi na namna anavyowatendea mema, mambo ya msingi, anavyoendelea kuboresha maisha ya

Watanzania. Mwenyezi Mungu ampe afya na umri mrefu aendelee kututumikia kwenye Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizo hizo pia zinakwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais kufikia malengo yake, vilevile Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu, kwa namna alivyoshiriki kikamilifu kumsaidia Mheshimiwa Rais. Pia, ninakupongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bajeti hii ni bajeti kama ambavyo Wabunge wenzangu walisema, ni bajeti ya mwisho kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili, lakini ni bajeti ya wananchi. Tunapozungumza kwamba hii bajeti ni ya wananchi ni kweli kabisa hii bajeti ni ya wananchi, inakwenda kujibu matakwa ya wananchi, inakwenda kuboresha maisha ya wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Watendaji wake tunawashukuru sana. Pia pongezi hizi kwa Katibu wa Wizara hii kwa namna wanavyochapa kazi kumsaidia Mheshimiwa Waziri ili kufikia hapa tulipofika leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pongezi siziwezi kuacha kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Mimi amenilea kwenye Bunge hili zaidi ya miaka 10 leo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Pia ninakushukuru Naibu Spika kwa namna anavyoliongoza Bunge letu na kututendea haki sisi Wabunge, tunaweza kudumu hapa Bungeni. Nisiwasahau vilevile Wenyeviti wetu wa Bunge ambao wao nao wako bega kwa bega kutusaidia kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Tulia ili kuendesha Bunge vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa miaka 10 leo, sitaacha kuwapongeza watumishi wote wa Bunge hili kwa namna walivyotuhudumia tangu tumeingia kwenye Bunge hili na tunakwenda kuhitimisha Bunge la Kumi na Mbili. Vilevile na wahudumu wetu kule nje mwa benki, Benki za *NMB, CRDB, NBC,*

na AZANIA, kwa namna wanavyotuhudumia, kwa ujumla ninasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu akijaalia mwezi Novemba tutakutana tena hapa, kwani Wanaliwale bado hawajachoka. Wanaona Mbunge wao ninawatumikia vizuri na wataendelea kunipa imani hii, ninategemea hilo. Kwa hiyo, Ndugu zangu miaka 10 siyo haba, mimi kama Zuberi yapo niliyopatia na yapo niliyokosea, lakini yote haya ni ubinadamu. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimetanguliza shukrani? Nimetanguliza shukrani kwa sababu ya utekelezaji ulio bora wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Mimi ndiyo niliyokabidhiwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwenye Halmashauri au Wilaya ya Liwale kuomba kura kuitangaza hatua kwa hatua na hapa ninasema kwamba Ilani imetekelezwa zaidi ya 95%, kwa hiyo, hasa kwa upande wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa kilimo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sasa hivi ni mwaka wa nne mfululizo sisi wananchi wa Liwale au kwa Mkoa wa Lindi kwa ujumla wetu tunapata pembejeo bure pembejeo za kilimo, ile ni dhahabu ya Kusini, tunashukuru sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu siyo tu kwa kutupatia pembejeo za kilimo bure, lakini na uboreshaji wa bei. Kwa kweli sasa hivi hali imekuwa ni nzuri kidogo, kwa hiyo jambo hili ni jambo la kushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine inayofanya ninaendelea kushukuru ni tangu nimeingia kwenye Bunge hili kilio changu kikubwa ilikuwa ni Barabara ya Nangurukuru – Liwale, Barabara ya Nachingwea – Liwale. Ninashukuru mwaka huu nimeiona, kwenye bajeti hii nimeiona na Barabara yangu ya Nachingwea – Liwale, Masasi – Liwale kilometa 175, mwaka huu nimeiona inakwenda kuanza kilometa 55, hili ni jambo la kushukuru sana. Ninamwomba Mwenyezi Mungu na iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nangurukuru – Liwale kilometa 230. Mwaka huu tumetengewa kilometa 72 na kwa kuanza kwa mwaka huu tunakwenda kuanza kilometa 10. Jambo hili ni jambo la kushukuru sana na niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais na ninaendelea kuishukuru Serikali sikivu ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wafugaji sisi katika Mkoa wa Lindi ndiyo Wilaya ambayo tulikubali kupokea wafugaji kutoka kule Ihefu. Ninaomba hapa napo niendelee kuwashukuru sana mwenye Wizara hii kwa namna anavyotutendea haki. Hapa niendelee kusisitiza, shida kubwa ya kuhama Ihefu iliyowapeleka Liwale ni kufuata malisho, kwa maana ya majani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli malisho yapo ya kutosha lakini wafugaji wale bado wanahangaika na masuala ya maji. Ndiyo maana wanahangaika, utakuta barabarani kiangazi wanahama kutoka Liwale wanaenda Rufiji, masika wanarudi Liwale. Ninaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hapa tuanagalie namna ya kuwapatia maji wafugaji wale ili wapunguze kijiji kile ufugaji wa kuhamahama, wabaki kule Liwale kama malisho yanawatosha na kwa sababu sisi tayari kule tumeshatengeneza mpango kazi wa kupanga eneo la wafugaji na eneo la wakulima ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali migogoro ile sasa inaendelea kupungua, ingawa bado haijakwisha, lakini inaendelea kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru watu wa Maliasili. Watu wa Maliasili tulihangaika sana hapa na jamii ya tembo na kweli juhudi zinaonekana, Ndege Nyuki tunawaona na wale vijana wa *VGS* kweli kabisa kwenye vijiji vyetu vijana kadhaa wamechukuliwa wamekwenda huko *VGS* kwenda kujifunza namna ya kuishi na wale wanyama, lakini kikubwa zaidi, mwezi uliopita tumepokea kifuta machozi, ingawaje unajua siyo kwamba kimekidhi haja kwa watu wote walioathirika, lakini

angalau inaonyesha juhudi kwamba Serikali inawajali watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wamelipwa watu zaidi ya 2,690, wote hawa wamepata kifuta machozi na ndiyo maana kwenye hotuba yangu nikatanguliza kushukuru, kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema, asipomshukuru mwanadamu mwenzie basi hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani hizi nimezielekeza kwa namna ambavyo sisi Wilaya ya Liwale kwenye kipindi hiki cha miaka mitano tumeweza kujenga shule za sekondari mpya tano, vilevile tumejenga vituo vya afya vya kisasa kabisa vitano, pia tumejengewa hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hospitali peke yake au vituo vya afya peke yake, vipo vifaa vya hospitali ambavyo zamani sisi pale unaweza kwenda kuvikuta Muhimbili au uende Sokoine au uende hospitali ya rufaa, lakini leo vifaa hivi vipo kwenye hospitali ya Wilaya ya Liwale. Kwa hiyo, tunapoendelea kuisifia Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, tunaisifia tunamaanisha na kweli tofauti zinaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa maneno haya ninashukuru sana na naiunga mkono bajeti hii na ninawatakia kila la heri. Wabunge wote walioko kwenye Bunge hili tumwombe Mwenyezi Mungu mwezi Novemba tukutane hapa wote tukiwa salama kama ambavyo mimi wananchi wa Liwale wamenihakikishia kwamba watanirudisha na ninawaombea Wabunge wote walioko humu ndani warudi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kaijage, jiandae Mheshimiwa Mwakibete. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami kupewa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na mimi leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia bajeti hii. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake, kwa kipindi cha miaka minne wamefanya kazi kubwa sana ya kuliongoza Taifa letu na kuwaletea Watanzania maendeleo, akisaidiwa na wasaidizi wake wote, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitofauti sana utulivu wa nchi yetu umechangiwa na uimara wa vyombo vya ulinzi, vikiongozwa na Amiri Jeshi yeye Mkuu, ninavipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana nipongeze uongozi wa Bunge ukiongozwa na Spika mahiri sana, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti na Watumishi wote wa Bunge. Wamefanya kazi kubwa sana kuongoza Bunge hili kwa kipindi ambacho tumekaa humu ndani, wapokee pongezi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ama Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea sana kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi katika Taifa hili katika ujenzi wa uchumi, uzalishaji na utoaji huduma kwa Watanzania, hii yote ni kutokana na uimara na maelekezo mazuri ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika Ibara ya 128, 129, na 130 ambayo Serikali inatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeielekeza Serikali kuendelea kutoa mazingira mazuri ya vyama vya wafanyakazi, wafanyakazi na waajiri ili kuwe na *harmony* kule mahali pa kazi ili mwisho wa siko maslahi ya wafanyakazi na haki zao ziendelee kuboreshwa kwa umoja huu ambao tunaita utatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka hii minne ambayo Mheshimiwa Rais amekaa madarakani, nikiwa kama mwakilishi wa wafanyakazi na Wabunge wenzangu wakinisaidia, wafanyakazi walikuwa wana changamoto nyingi sana, lakini tumeona jinsi ambavyo Serikali ya Mama Samia imefanya kazi kubwa sana na huo ndiyo moyo wa Mama Samia eneo la watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mengi sana ambayo tulishawahi kuchangia na wenzangu humu ndani, lakini leo nitaje machache tu machache ambayo Mheshimiwa Rais na Serikali yake wamewafanyia wafanyakazi wa Tanzania. Mojawapo ni kuwa, Serikali toka ameingia madarakani Mama Samia ameweza kupandisha madaraja watumishi zaidi ya 470,000, ametumia zaidi shilingi bilioni 689. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, Mheshimiwa Rais ameweza kulipa malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi na wale wastaafu. Kilikuwa kilio kikubwa, hakumaliza yote lakini amefanya kazi. Amelipa wafanyakazi na wastaafu na waliokuwa madarakani malimbikizo ya mishahara wanaotimia 187,000 na imemgharimu Serikali shilingi bilioni 318. Ni kazi kubwa Mheshimiwa Rais ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, Mheshimiwa Rais alivyoingia madarakani tu kilio kikubwa sana cha watumishi wale wa kima cha chini, mwaka 2022 akapandisha mshahara, kutoka 300,000 mpaka 370,000. Hakuishia hapo, juzi tu Mei Mosi mama amepandihsa tena. Kima cha chini kutoka shilingi 370,000 hadi shilingi 500,000. Huyo ndiyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, ameweza pia kuboresha pensheni. Sasa hivi bajeti ijayo wale kima cha chini wastaafu pensheni yao itaongezeka kutoka shilingi 100,000 mpaka 200,000. Amewakumbuka wastaafu hawa, maana maisha yanabadilika. Hawawezi kubaki kwenye mshahara huo huo pensheni hiyo wakati maisha yakienda yakibadilika. Huo ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais na Serikali kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, ametoa ajira nyingi zaidi ya 400,000, kuajiri siyo mchezo, *wage bill* kubwa inatumika, lakini tumeona nia yake ya kuongeza ajira kwa Watanzania. Ameanzisha hili suala la *BBT*, hii yote anajaribu kutanua wigo kwa vijana nao wapate ajira. Huo ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ameweza kurudisha watumishi kwenye utumishi wa umma waliotolea kwenye utumishi wa umma, amewarudisha zaidi ya 2,000. Huo ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais kwa watumishi na watumishi wa Tanzania wanasema Oktoba wanatiki kwa Mheshimiwa Dkt. Samia kwa maslahi bora ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, ameendelea kuongeza bajeti ya *OSHA*, ameongeza wafanyakazi. Hawa ni watu muhimu sana, wanakagua maeneo ya kazi ili watumishi wafanye kazi katika mazingira ambayo ni salama. Huo ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais kwa watumishi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, hata kuongeza au kuruhusu tena ile 10% ya mikopo kule kwenye halmashauri zetu, huo ni moyo wa Mheshimiwa Rais kukuza wale wajasiriamali wa kati na wa chini ili angalau wawe na ajira, wawe na kipato. Hiyo ni sehemu ya ajira kwa watu ambao wako kule kwenye biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, kwa moyo wake wa dhati alishauri, alipendekeza iundwe bodi, bodi ambayo itasimamia kima cha chini cha mishahara, sekta binafsi na sekta ya umma. Umma imefanya vizuri na juzi kwenye Mei Mosi tumemsikia akitamka, akiwaasa na kuwataka wale ambao wanasimamia upandishwaji wa kima cha chini cha mishahara sekta binafsi wafanye kwa haraka ili nao wasione wametengwa, watu wa sekta binafsi. Huo ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote aliyofanya hayo, bajeti hii ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri,

ninampongeza sana wanafanya kazi kubwa sana na Naibu Waziri, imeendelea katika vipaumbele vyake vya utekelezaji wa bajeti iliyopita. Moja ya kipaumbele kati ya vitano ilikuwa ni kuendeleza rasilimali watu ili kuhakikisha ufikiwaji wa malengo ya Dira ya 2025 unafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa habari njema sasa, hata juzi nimeangalia, katika bajeti hii waliyoisoma wameendelea kutekeleza kipaumbele hicho ambacho ni kuimarisha rasilimali watu hususan katika sekta ya huduma za jamii. Sekta ya huduma za jamii ina maana na afya iko hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema kidogo kwenye afya leo. Serikali ya Awamu ya Sita imewekeza sana kwenye afya, sana sana. Elimu kwa wabobezi, vifaatiba, miundombinu na kadhalika na kadhalika. Inastahili pongezi kubwa na bajeti hii tumeona ya afya imepanda kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana *TRA*, imefanya marekebisho ya TEHAMA na kutoa elimu na hamasa kwa wale wote wanaokusanya kodi ili mwisho wa siku pato la ndani liwe juu. Ninaipongeza sana *TRA* chini ya Kamishna mpya wa sasa hivi, lakini lazima sasa tufikie mahala *mindset* ya Watanzania ibadilike kutoka kwenye utegemezi wa afua za mambo ya afya kutoka kwa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tu-*finance* Wizara ya Afya, tui-*finance* kwa viwango vya juu, katika vipaumbele tunatoa vipaumbele mbalimbali. Ninashukuru kwamba kuna uwekezaji kwenye kilimo, mifugo na kadhalika, lakini hawa watu tunaowekeza huko kama watakuwa afya zao ni mgogoro au wanauguliwa magonjwa sugu, hakika ufanisi wao katika uwekezaji utakuwa ni wa chini. Kwa hiyo, moja kwa moja tunahitaji kuwekeza sana kwenye Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wahisani wengi sana wamejitoa kwenye mambo ya afya na utaona hizi *vertical program* nyingi zinaelekea ku-*collapse,* huo ndiyo ukweli. Kwa hivyo.....

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kidogo muda. Ni kwamba, tulikuwa tunategemea wahisani kwa mfano Marekani, sasa hivi Irani wanapigana, anawekeza nguvu kuwa-*support* washirika wake. Tumeona kwenye bajeti ya Ujerumani wametenga zaidi ya trilioni moja *Euro* wameweka Jeshini, atakukumbuka kukuletea vifaatiba huyu? Hawezi kukumbuka!

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ninachozungumza? Tuwekeze kwa hawa watu wanaitwa wahudumu wa afya ya jamii ya msingi. Kwa hiyo, hawa watatoa elimu chini ambayo itasawasaidia Watanzania wasifikie *complication*, wawahi hospitalini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwakibete wajiandae Mheshimiwa *Engineer* Samweli na Mheshimiwa Tecla.

Mheshimiwa *Eng*. Samweli, ngoja kwanza ngoja! Ulikuwa unafikiri nini, Jimboni? Eeh, acha Mawazo, mweke Mungu mbele Mzee. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Aah, *sorry sorry* ni Mheshimiwa Mwakibete, *Sorry*. Mheshimiwa Mwakibete. Hayupo, *okay* sawa, basi endelea.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Bajeti yetu Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kulihudumia Jimbo langu la Hanang kwa miaka mitano na hii ni

bajeti yangu ya tano ninachangia na ninaamini ni bajeti ya mwisho kwenye mpango wetu wa miaka mitano. Ninawashukuru sana wananchi wa Hanang kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakishirikiana na mimi, mara zote wamekuwa wakiniunga mkono wakati ninafanya shughuli zangu za Ubunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe pamoja na Spika, Wenyeviti wetu wa Bunge, kwani mara zote nikiwa na jambo la wananchi wa Hanang wamekuwa wakinipa nafasi niliseme hapa Bungeni na Wanahanang kwa njia hiyo wamesikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Watumishi wote wa Serikali, kwani mambo mengi ya Wanahanang ambayo nimepeleka Serikalini tumepata majibu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mheshimiwa Queen Cuthbert Sendiga, mara zote amukuwa akiiangalia Hanang kwa jicho la pekee, ninamshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Hanang Mheshimiwa Almishi Hazali, kwani amekuwa akiwahudumia wananchi wa Hanang na tumekuwa tukishirikiana naye. Ninamshukuru Mkurugenzi kwa kuwa miradi mingi ambayo inapelekwa Jimboni kwangu yeye amekuwa msimamizi mkuu na amekuwa akisimamia vizuri na watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kwa ushirikiano ambao tumekuwa tukifanya kazi nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano huu ambao nimeupata kutoka Serikalini umewezesha kwenye sekta ya miundombinu ya barabara kufungua Barabara ya Waama – Mureru kupitia Diloda, Barabara ya Hirbadaw – Mwanga, Barabara ya Mogitu – Gendabi. Tumeweza kufungua Barabara ya Dawar kwenda Ziwa Chumvi, Barabara ya Mulbadaw Kibaoni kwenda Bassodesh, Barabara ya Gijetamohog kwenda Garawja, Barabara ya CMC kwenda Bassodesh, lakini tumefungua barabara za lami kwenye Mji wa Kateshi. Pia tumejenga Stendi kubwa ya Kisasa pale

Kateshi, Stendi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na stendi ile sasa inatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sekta ya Maji, ushirikiano nilioupata Serikalini umewezesha Mji wa Katesh kuwa na maji; pale imewekwa zaidi ya shilingi bilioni 10. Tumetekeleza Mradi wa Maji ambao unaenda Kata ya Gehandu na maeneo ya jirani, mradi ambao kwa sasa umefikia 80%. Wananchi wa Gehandu wanapata maji, yamebaki maeneo machache ambayo yanatakiwa yapelekewe maji ikiwepo eneo la Gidabwanja, Marega, Mwanina na Milongori.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetekeleza Mradi wa shilingi bilioni 16 wa Ziwa Bassotu ambao kwa sasa umefikia kwenye 48%. Pia, tumeanza kutekeleza Mradi wa Bwawa la Bassotughang pale ambapo maji yameanza kutumiwa na wananchi na mradi ule unaendelea. Baada ya mradi ule kukamilika utahudumia Kata ya Dirma, Wareta, Simbay na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano huo pia umeondoa adha ya maji kwenye maeneo ambayo yalikuwa korofi kama eneo la Backchand ambayo ipo kata ya Masakta pamoja na eneo la Basodami ambalo lipo Kata ya Balangdalalu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye umeme tulikuwa tuna vijiji 46 havikuwa na umeme, lakini sasa vijiji vyote vina umeme. Pia, vitongoji 64 vimepelekewa umeme, njiani tunavitarajia kupata vitongoji 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Sekta ya Afya tumejenga vituo vipya vya afya saba. Pia, tumeboresha hospitali yetu ya Wilaya ya Tumaini na tumejenga zahanati zaidi ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye elimu tumejenga shule mpya za sekondari karibu sita, lakini tumejenga madarasa na tumejenga maabara. Maana yake Sekta ya Elimu nayo imekuwa bora. Ukiacha kujenga na kuboresha elimu ya msingi na elimu ya sekondari, tumejengewa Chuo cha *VETA* pale Nangwa na shughuli inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri yote haya ambayo yamefanyika kwenye eneo letu, Wanahanang wamenituma nimwombe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais msikivu ambaye mara zote amekuwa akisikia kwamba barabara zetu kwa sasa nyingi zimekuwa korofi. Kwa mfano, Barabara kuu inayotoka Babati kwenda Singida, eneo la Dareda kwenda mpaka Gehandu mashimo yamekuwa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile sasa kwa sababu ya mazingira na ubovu wake imekuwa ikisababisha ajali nyingi kwa sababu watu wanakwepa mashimo wanaenda pembeni mwa barabara. Pia, wananchi wanaotembea kwa miguu wamekuwa wakipata adha. Tuna barabara nyingi ambazo kwa kweli kwa sababu tumepata mvua nyingi zina hali ambayo si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais mpenda watu, Rais mbunifu na alibuni ile *bond* ya miundombinu kwa kushirikiana na *CRDB* na kwa kuwa zilishakusanywa fedha za kutosha, zile fedha sasa zitoke. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri, tunaomba zile fedha sasa zitufikie kwenye majimbo yetu, zile fedha zikakarabati barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliomba shilingi milioni 831 kwa ajili ya Barabara ya Mogitu kwenda Balangdalalu ambayo kwa sasa kama imekuwa njia ya maji. Watusaidie kwa sababu hiki ni kipindi cha mavuno na wananchi wanataka wakavune mazao yao na kuyasafirisha. Barabara ya Endagaw - Gidahababieg nayo imekuwa na makorongo mengi na haipitiki vizuri kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tuna barabara zetu zile ambazo ziliathirika wakati wa maporomoko ya Mlima Hanang. Kuna Barabara ya Endasak – Dawar na barabara ya Jorodom - Nangwa – Gitting; barabara hizi zina hali mbaya. Pia, barabara za Mji wa Katesh na barabara za Ganana tunaomba tusaidiwe zile fedha zikitoka mapema barabara zile zikakarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, uchumi wa wananchi utachangamka kwa sababu wananchi wa Hanang ni

wakulima wazuri na kwa hakika miundombinu ya barabara ni sawa na mishipa ya damu kwenye mwili wa binadamu; popote pale ukipata changamoto ya mshipa hutapata usingizi. Uchumi wa Hanang kwa sasa haupati usingizi kwa sababu ya changamoto ya miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yote mengi yamefanyika mazuri, lakini kwa kuhitimisha tunavyoenda kwenye Ilani mpya tunayoenda kuinadi, tunayo barabara yetu ambayo tumekuwa tukiisema mara nyingi (Barabara ya Haydom – Mogitu). Barabara hii imeshafanyiwa usanifu wa kina na upembuzi yakinifu. Tunaomba fedha zitoke kwa ajili ya kuwalipa fidia wale ambao wataathirika ili barabara ile ianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati barabara hiyo inajengwa, tuangalie namna ya kujenga barabara chache za Mji wa Bassotu kwa sababu ule ndiyo mji mkubwa kwa maana ya Wilaya ya Hanang ndio eneo ambalo lina watu wengi. Tuangalie namna pia ya kujenga barabara za lami kwenye Mji wa Endasak, tuone namna ya kuendelea kujenga na kuboresha barabara za lami katika Mji wa Katesh na tuendelee kupeleka huduma za maji kwenye maeneo ambayo bado hatujafikia kwa namna ya kuunganisha vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji mengi tunayapata kwenye visima virefu, inavyoharibika *pump* wananchi wanakosa maji. Tuone namna ambavyo tunaweza kuunganisha vyanzo mbalimbali ili angalau tuweze kuwa na changamoto upande mmoja, upande mwingine uweze kupata maji na wananchi waendelee kupata maji muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikia Wabunge wenzangu wakisema tutengeneze gridi ya maji. Tutengeneze gridi ndogo ndogo za maji ili kwamba upande mmoja ukiwa na shida upande mwingine uendelee kupata huduma. Kwa namna hiyo tutadhibiti suala la wananchi kukosa maji chanzo kimoja kikiwa na changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe hotuba yangu leo kwa sababu ndiyo mara ya mwisho nikisimama hapa Bungeni na nikipata nafasi labda kwenye maswali ya nyongeza na nini, niwashukuru sana wananchi wa Hanang. Sisi tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametufaa kwa mengi. Tulipata changamoto ya maporomoko ya Mlima Hanang, wengi ni mashahidi Serikali yote ilihamia Hanang na ilihamia Hanang kwa sababu ya upendo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliona shida yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema inapofika Oktoba tutalipa fadhila kwa mema ambayo ametutendea na Wabunge wenzangu wamekuwa wakisema sisi ikifika Oktoba hatuna mjadala, tunatiki kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wananchi wenzangu wa Jimbo la Hanang, nimewatumikia kwa muda ambao unakaribia miaka mitano. Kijana wao bado nina nguvu, nipo na nitaendelea kuomba idhini ya kuwatumikia tena. Wakati utakapofika tutayasema ya kwetu, tufanye kazi ya kuletea maendeleo Jimbo letu la Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni:-

Wageni 87 wa Mheshimiwa Felista Njau, wanafunzi na Walimu wa shule ya Msingi Ebenezer kutoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni 75 wa Mheshimiwa Michael Kembaki, wanafunzi na Walimu wa shule ya *Ghati Memorial* kutoka Babati, Mkoani Manyara. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Wapo Walimu 10 na wanafunzi 100 wa Shule ya Awali na Msingi ya *Kingdom Heritage* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo Walimu nane na wanafunzi 66 wa Shule ya Sekondari Anazak kutoka Kibaha, Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge, anaomba kuwatangazia na kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuhusu kushiriki Tamasha la Michezo na Burudani *(Grand Bunge Bonanza)* litakalofanyika siku ya Jumamosi tarehe 21 Juni, 2025 katika viwanja vya shule ya Sekondari ya John Merlin iliyopo Miyuji Jijini Dodoma.

Tamasha hili litahusisha timu za Bunge na wadau wengine na litakuwa na michezo mbalimbali kama ifuatavyo: Mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa wavu na kuvuta kamba. Michezo ya burudani ni kama ifuatavyo: Riadha, kukimbia na gunia, mchezo wa bao, kufukuza kuku, kupenya kwenye mapipa, kuruka kamba na kuvaa soksi.

Waheshimiwa Wabunge wote mnahimizwa kushiriki kikamilifu Bonanza hili ambalo litaanza saa 11 asubuhi.

Ninamwita Mheshimiwa Tecla, jiandae Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipatia afya njema lakini pia kwa kuniruzuku uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru jamii yangu ya Mkoa wa Lindi kwa kuniamini kuwawakilisha kwa muda huu wa miaka mitano. Ninawashukuru sana kupitia Chama Cha Mapinduzi na ninaamini kabisa tutaendelea kufanya kazi kwa kipindi kijacho kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotupatia uhai. Mimi ndugu yao Tecla Mohamedi Ungele, ninaendelea kufanya

kazi ya kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Wizara ya Mipango na Uwekezaji, lakini pia Wizara ya Fedha. Timu yote hiyo wamefanya kazi vizuri na wanaendelea kufanya kazi kubwa sana ya kuendeleza na kumsaidia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yangu ninaielekeza kwenye maeneo mbalimbali; eneo la kwanza kwenye Sekta ya Afya. Tunajua afya ni mtaji na hili Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi na ametekeleza kwa kiasi kikubwa sana na kwa kiasi chote kule Mkoa wa Lindi. Tulikuwa na hospitali ya Mkoa (hospitali ya Rufaa), amejenga hospitali kubwa ya Rufaa kule maeneo ya Mitwero; tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, amejenga hospitali ya Manispaa ya Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hospitali nyingine pia maeneo mengine ya wilaya nyingine kulikuwa hakuna hospitali za wilaya, tumemsikia Mheshimiwa Kuchauka, Wilaya ya Liwale kulikuwa hakuna hospitali ya wilaya walikuwa kwenye kituo cha afya tu, lakini kuna hospitali ya wilaya tayari. Pia, hata Ruangwa kuna hospitali ya wilaya na Jimbo la Mtama kuna hospitali ya wilaya pia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amepeleka pia vifaa, vitendea kazi na vifaatiba kwenye maeneo hayo. Hata hivyo sisi wana Lindi tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuletea huduma za tiba za huduma za dharura kwenye Hospitali ya Ruangwa, Kinyonga pale Kilwa lakini pia na Liwale. Pia, tunashukuru ametuletea huduma ya *ICU* (kuhudumia wagonjwa mahututi) pale hospitali ya Wilaya ya Nachingwea. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ametuletea *ambulance* 13 vile vile katika kipindi chake cha miaka minne ambapo kila wilaya

imepata *ambulance* mbili. Zilikuwepo zingine lakini kipindi chake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameziongeza hizo 13 pamoja na hiyo moja ya hospitali ya Mkoa. Hatujawahi kuyaona haya huko miaka mingine iliyopita. Huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunayemfahamu sisi Wanalindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwakilishi wangu hapa Bungeni mimi nikiwa mtaalam wa afya pia nilipigania sana mafunzo haya ya *community health workers* yarudishwe tena. Kweli yamerejeshwa lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, naye katika programu yake ya *community health workers* kwenye mikoa ile 10 tunaona Mkoa wa Lindi ni mmojawapo katika hiyo programu ya *Community Health Workers.* Sasa hivi *Community Health Workers* kwa Mkoa wa Lindi inatekelezwa Manispaa ya Lindi na Mtama pamoja na Ruangwa. Tumeona vijana wameajiriwa kule wanaendelea kufanya kazi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Community Health Workers* ni muhimu, hao wanakuwa *linkage* kati ya jamii na idara ya afya. Wanafanya huduma ya kushauri, lakini kwa kiasi kikubwa kwenye kuzuia magonjwa yasiyoambukiza. Pia kushauri akinamama kwenda kliniki kuhudhuria chanjo na kadhalika. Kwa hiyo kwa kiasi kikubwa idara hii ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona sisi Mkoa wa Lindi pia tumetekeleza ile programu ya M-Mama ile ya kumuwakilisha mama kuhakikisha anapata rufaa ya kwenda kwenye huduma za afya (mama mjamzito na mtoto chini ya siku 28). Tunaona hii ndio iliyopunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka 550 kwa kila vizazi hai 100,000 mpaka kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka huu 2025 kuanzia pale tulipotoka 2020. Sisi Wanalindi, tunashukuru sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sekta ya Elimu pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya mambo makubwa Mkoa wa Lindi. Amejenga Shule ya Sekondari ya Wasichana kubwa kule maeneo ya Kilangala iliyogharimu shilingi bilioni 4.5. Tunashukuru sana na miaka miwili iliyopita Mheshimiwa Rais, alipitia alienda kwenye ile sekondari na akaahidi, tukawa na

kilio cha kuomba barabara ya lami. Ninakumbuka Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo Mama Salma Kikwete aliomba na kweli sasa hivi tunajengewa ile barabara ya lami kutoka hapa Kilangala barabarani kwenda kule kwenye sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia anajali watoto wa kiume. Kunajengwa sekondari kubwa ya wavulana ya Kanda ya Kusini (Mtwara, Lindi na Ruvuma) inajengwa pale Kiwalala katika Jimbo la Mtama inaenda kugharimu shilingi bilioni 4.5; huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo sisi Wanalindi na Mtwara hakutuacha, anatupatia pembejeo bure kwenye zao la korosho. Huu ni mwaka wa nne na ndiyo imeongeza hata mapato ya korosho. Hilo ni jambo kubwa sana na hata bei imekuwa nzuri, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanalindi vilevile tunafaidi maji. Maji yanatoka Mavuji kwenda Nangurukuru, itaenda Kivinje na mpaka Kilwa Masoko. Pia, maji yanatoka Ng'apa kwenda mpaka Mchinga. Wana Mchinga sasa hivi wanakunywa maji ya kwenye bomba, maji safi na salama, huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maji kutoka Nyangao kwenda Ruangwa na baadhi ya vijiji vya Nachingwea tuna mradi mkubwa pia kule. Hata hivyo kwenye hotuba ya Wizara ya Maji walionesha kwamba wamefanya utafiti maji ya Mkoa wa Lindi na Mtwara yana *manganese*, madini ya chuma pamoja na chumvi. Kwa hiyo, sisi wana Lindi tunaomba mradi ule mkubwa wa kutoa maji kutoka Rufiji kuja Lindi na Mtwara, hilo jambo litakuwa ukombozi mkubwa sana kwa sisi Wanalindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanalindi tunasema hivi, itakapofika Oktoba (tena tunaona inachelewa tu), sisi tunatia tiki kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mambo haya aliyotufanyia ni makubwa hayajapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza sana Wizara hii na katika maeneo yao Wizara hii ya Fedha na Wizara ya Uwekezaji wamefanya kazi kubwa sana walivyokuja kwenye kubuni mfumo huu wa kodi ya tozo kwa ajili ya kugharamia na kudhibiti maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kugharamia bima ya afya kwa wote... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Gulamali, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo na Mheshimiwa Mulamula.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na kuwa sehemu ya kuchangia katika hii Bajeti Kuu. Kwanza niipongeze Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo imeifanya kwa kipindi cha miaka mitano; hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tanzania wote wameona kazi kubwa ambayo imefanyika katika maeneo mbalimbali na tumeshuhudia utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo ilikuwa inaendelea kutekelezwa katika nchi yetu kwenye Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Mawasiliano, Sekta ya Maji na Sekta ya Umeme. Tumeona kila *angle* fedha wamepeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana tulipitisha hapa Bungeni bajeti ya shilingi trilioni 50.2 na Wizara leo imekuja kutuambia tumekusanya shilingi trilioni 45 kutoka mapato yote, maana yake tumekaribia kufikia lile lengo. Vilevile, fedha hizi nazo tulizopitisha mwaka jana tulikuwa Wabunge wote hapa, tulipitisha bajeti hii shilingi trilioni 50.2, maana yake Wabunge tulichambua, tukaridhia na tukaipitisha kwa maana kwamba Serikali iende ikafanye kazi. Pia, mwaka huu Serikali imekuja imeliomba Bunge

tupitishe bajeti ya shilingi trilioni 56 na hapa tunaijadili na kuchambua. Maana yake tukimaliza tukapitisha, maana yake tumeiruhusu Serikali iende ikafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza kwa kazi kubwa ambayo imefanya. Inatokea unaweza kuona mtu mmoja miongoni mwetu Mbunge anatoka nje anasema Serikali inakopa sana hatuoni fedha inapoelekea. Sasa unabaki unashangaa tulikaa humu Bungeni, tukapitisha wote bajeti. Kwa mfano katika shilingi trilioni 50, uwezo wetu wa kukusanya mapato yetu ya ndani kupitia Serikali yetu tunakusanya shilingi trilioni 30, mwaka jana tumekusanya shilingi trilioni 30 na zilizobakia hizi 15 tumekopa ambazo hizo tumekopa ndani na nje ya nchi yetu na sisi tulipitisha na tumeruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wetu wa kukusanya mwaka 2020 tulikuwa tunakusanya bajeti yote kwa mapato ya ndani shilingi trilioni 20, lakini leo uwezo wetu wa kukusanya Serikalini umeongezeka, tunakusanya zaidi ya shilingi trilioni 30. Hongera sana Wizara kwa kazi nzuri na mikakati mbalimbali waliyoiweka. Kutoka shilingi trilioni 20 mpaka kufika shilingi trilioni 30 kukusanya kwenye mapato yetu ya ndani ni kazi kubwa imefanyika; hongera sana. Waongeze mianya ambayo tunaweza kupata fedha ili uwezo wa kujihudumia uongezeke. Ninapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anahoji uwezo wetu wa kukusanya shilingi trilioni 30. Kwa mfano kwa mwezi, mwaka 2020 tulikuwa tunakusanya shilingi trilioni 1.7, leo tunakusanya kwa mwezi shilingi trilioni 2.8. Maana yake ni kazi kubwa imefanyika, lakini fedha hizi tunazozikusanya katika hizi shilingi trilioni 2.8, trilioni moja peke yake inaenda kulipa mishahara ya wafanyakazi ambao hao wafanyakazi wanaoenda kulipwa mishahara tunawaajiri sisi na kila siku tunasema hapa tuongeze ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo anapokuja mtu anatokea anasema anashangaa; unashangaa vipi wakati tunapoajiri maana yake tunaongeza wigo mpana wa kulipa mishahara? Kama tunaongeza wigo mpana wa kulipa mishahara

(shilingi trilioni moja inaenda kwenye mishahara), shilingi trilioni moja tunaenda kulipa deni, maana yake katika shilingi trilioni 2.8, shilingi trilioni mbili zimeshatumika tayari na shilingi milioni 800 zinabaki kuhudumia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi ya maendeleo ni fedha ambazo tunakopa tunatekeleza. Ninaiomba Serikali iendelee kwa sababu hizi fedha zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ninaweza nikasema ni Wizara mwaka 2000 kwenye ile mahafali ya 43 ya *Open University* yaliyofanyika Kigoma ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais akamtuma Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika hotuba ya Mkuu wa Chuo aliiomba Serikali yale madeni yaliyokuwa yamehakikiwa yalipwe, kwa mfano ya madaktari na maprofesa wa vyuo vikuu kwa sababu, imekuwa ni muda mrefu kabla ya Bunge hili halijakwisha. Tunaomba Wizara ya Fedha iwalipe fedha zao hawa madaktari na maprofesa wa vyuo vikuu kwa sababu, walihakiki, kilichobaki ni utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara, bahati nzuri Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara amekuwa analisemea jambo hili mara zote kwa hiyo, ninampongeza kuwa mstari wa mbele. Ninaiomba Serikali iwalipe hawa madaktari pamoja na maprofesa wa vyuo vikuu, ili waendelee, wengine wamestaafu na wengine wamefariki, tunaomba haki zao waweze kupewa. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha wahakikishe wanawapa hawa watu stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niweze kusema ninawapongeza sana, kazi kubwa imefanyika, Serikali imefanya na miradi mikubwa inaendelea. Tunaona leo kuna uzinduzi wa Daraja kubwa la Kigongo - Busisi kule Mwanza, fedha nyingi zimetumika, hawa ndiyo ambao wanakusanya na wanapeleka kwenye utekelezaji. Ninaomba hii miradi yote, kwa mfano treni ya umeme ambayo tayari imefika Kigoma na tunajua kuna wakandarasi wapo kutoka Kigoma, Dodoma kwenda Tabora, Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza na Tabora kwenda Kigoma na Tabora kwenda Katavi, wawalipe wakandarasi ili kazi ifanyike na

mwaka 2028 Watanzania watembee, wafurahie matunda ya nchi yao kwa kutumia treni ambayo itarahisisha kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Serikali inafanya kazi na sisi Wabunge tunawaunga mkono, hasa kwa kupitisha hii bajeti kuu. Wachape kazi, sisi Wabunge tunawaunga mkono na tunasema kwamba, miradi yote inayotekelezwa na wanayoifanya Watanzania wanaiona katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu tunahitaji umeme vitongojini, tunaona wakandarasi wameanza kuingia kwenye maeneo yetu na kazi inafanyika. Tumepewa awamu hii vitongoji 86, lakini uhitaji ni zaidi ya vitongoji 86. Tunaiomba Serikali kwa sababu, tunapitisha bajeti hii fedha zinazotoka kwenda kwenye miradi ya umeme vijijini tuipate kwa wakati, wakandarasi waje kwenye *site,* wananchi waweze kupata huduma ya umeme kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya maji, pia tumeona miradi mikubwa inafanyika nchi nzima maeneo mbalimbali. Sisi watu wa Manonga tumepata miradi mikubwa ya maji ya fedha za kutoka Benki ya Dunia, hizo ndiyo fedha za mikopo, lakini zinakuja kufanya kazi, kwa ajili ya wananchi wetu. Mtu anasema fedha hizi za mikopo hatuoni zinapoenda. Zinaenda kwenye miradi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kwangu tumepata fedha hizi za Benki ya Dunia ambazo zinatekeleza Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria, kutoka Ziba kwenda Ndembezi, kutoka Ndembezi kwenda Nkinga, kutoka Nkinga kwenda Mizanza – Mwisi, kutoka Mwisi mpaka Simbo na bado tutaomba tena fedha nyingine zitengwe kutoka Simbo kwenda Igoweko, kwenda kule Tambalale na kwenda Uswaya kwa sababu, wananchi wanahitaji huduma. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iendelee kufanyia kazi suala la mikopo, deni letu ni himilivu na tunaweza kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeweza kulipa mwaka huu trilioni 11 na sasa hivi hapa tunapitisha bajeti ya kwenda

kulipa mwaka unaokuja shilingi trilioni 14 maana yake nchi yetu ni himilivu, inaweza kulipa deni, inakopesheka na inaaminika kwa sababu, tunakusanya tunalipa, tunakusanya tunalipa. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge tunasema chapeni kazi, chukueni fedha tekelezeni miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wanasema hawaoni inakotekelezwa miradi, hawaoni fedha zinakoenda, maana yake ni kwamba, hawafuatili hata bajeti zinazowasilishwa hapa Bungeni. Kama unafuatilia hauwezi kuhoji masuala ambayo yanatekelezwa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, hayupo. Mheshimiwa Balozi Mulamula, wajiandae Mheshimiwa Kapinga na Mheshimiwa Saputu.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwenye hoja mbili zilizo mbele yetu, yaani Bajeti za Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na walionitangulia kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa kuandaa na kutuletea bajeti inayoakisi uhalisia wa mahitaji ya wakati tuliopo, inayojielekeza kujibu changamoto za Taifa letu na iliyojaa umadhubuti kwa kukabili changamoto za hali ya uchumi wa dunia na kujenga ustahimilivu wa uchumi wetu *(resilience)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuwasilisha bajeti za maeneo yao kwa umahiri mkubwa. Kipekee

ninampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, kwa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali. Ninawapongeza Naibu Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, ambao naona wamekaa kama mapacha hapo na timu za Wizara zote mbili kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wasemavyo supu hunywewa ikiwa ya moto, hivyo nianze kwa kusema ninaunga mkono bajeti hii. Sababu za kuunga bajeti hii ni tatu. Kwanza kabisa, ni bajeti inayotujengea uhimilivu *(resilience),* pili, ni bajeti inayolenga kujenga uchumi shirikishi *(inclusive economy)* yaani kutomwacha mtu wala sekta yoyote nyuma *(leaving no one behind)* na tatu, ni bajeti inayothubutu kuongeza kasi ya kukuza uchumi wetu *(disruptive growth)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza na bajeti hii inatujengea uhimilivu kwa kuongeza nidhamu katika makusanyo na matumizi ya fedha za ndani. Bajeti hii inapunguza utegemezi wa misaada kutoka nje. Dhoruba tulizopitia hapo katika kipindi cha *COVID* au UVIKO-19, Vita vya Urusi na Ukraine iliyochochea kupanda kwa gharama za vyakula na bei ya mafuta na *logistics,* kuadimika kwa Sarafu ya Dola ya Marekani nchini na hatimaye kuondolewa kwa msaada kutoka Marekani na kupungua misaada kutoka Ulaya zimetufundisha kujihami na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahishwa kwamba, Serikali itatenga bajeti katika muda wa kati itakayolenga kuziba pengo la fedha zilizokuwa zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa wabia wa maendeleo, hususani mataifa makubwa ambayo yamepunguza au kusitisha misaada iliyokuwa inatolewa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali zaidi katika eneo la afya. Hadi sasa Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 82 kuziba pengo litokanalo na mabadiliko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie tena kwamba, taasisi mojawapo iliyoathirika na kusitishwa kwa miradi hiyo ni Taasisi ya Benjamini Mkapa *Foundation,* ambayo ilikuwa inatekeleza mradi mkubwa wa afya endelevu kupitia msaada wa Shirika la Maendeleo la Marekani ambalo limefungwa na kusitisha misaada yote na kuathiri wafanyakazi na wataalam wapatao 1,296 ambao wanatoa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya vya umma vipatavyo 701 kwenye mikoa yote 22 ya Tanzania Bara na mikoa mitano ya Zanzibar ambao wote wamepoteza ajira. Ni matumaini yetu kwamba, bajeti itakayotengwa na Serikali itasaidia katika kuwarudisha kazini watumishi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema pia, nimefurahishwa na maboresho ya mfumo wa kodi, mapendekezo ya kodi mpya na nafuu katika baadhi ya kodi zenye lengo la kuchochea uwekezaji wa ndani, wepesi wa kulipa na kuongeza matumizi ya kidigitali katika ukusanyaji wa mapato unaotuongezea uhimilifu kwa kuvutia uwekezaji wa ndani. Nimependa uamuzi wa kuongeza kodi kwenye michezo ya kubahatisha, *betting* na maeneo mengine, ili kupata fedha, kwa ajili ya kufikia pengo la msaada kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavutiwa zaidi na uamuzi wa kupunguza *VAT* kutoka 18% hadi 16% kwa malipo yatakayofanyika kwa njia ya mtandao. Ninafurahishwa na dhima ya kuimarisha ubora wa elimu anayopewa mtoto wa Kitanzania na siyo bora elimu, baada ya upatikanaji wa elimu. Hivyo hivyo kwamba, Serikali inakwenda kwenye *modernization* ya shughuli za uzalishaji kilimo bora, ufugaji na uvuvi wa kisasa pamoja na kuongeza thamani ya mazao ndani ya nchi na kuongeza ujenzi na upanuzi wa viwanda. *This is the way to go. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uchumi shirikishi, ripoti kadhaa huko nyuma zimeonesha kwamba, pamoja na uchumi wetu kukua, ukuaji huo ulikuwa haukui sana kwenye sekta zinazoajiri au kugusa watu walio wengi. Katika bajeti hii unaiona dhamira hiyo kwenye kupunguza kodi kwa pikipiki na bajaji ambazo ni ajira za mpito kwa vijana wetu na kuondolewa kodi

kwa mbolea inayozalishwa nchini na kuweka kodi kwenye baadhi ya bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki, ili kulinda viwanda vyetu vya ndani. Kwa ujumla wake bajeti inatoa unafuu na mwanya mkubwa kwa biashara na huduma zinazozalishwa na wawekezaji wa ndani, ili kuwezesha sekta binafsi kushiriki zaidi, kupanuka zaidi na kuajiri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia, kusema katika uthubutu wa kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, bajeti hii tunatarajia itupeleke kwenye ukuaji wa uchumi wa asilimia sita kutoka 5.5 kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee kwa kifupi, kutokana na ufinyu muda, utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ambayo imegusiwa kwa kifupi kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali. Pamoja na kutambua mafanikio ya diplomasia ya uchumi katika kuchangia kwenye kukuza maendeleo ya nchi yetu rai yangu ni kwamba, Serikali iwe na mkakati wa Kitaifa katika utekelezaji wake maana ni suala mtambuka, haliwezi kuachiwa tu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pekee yake. Ili kufanikisha sera hii, balozi zetu zinahitaji rasilimali fedha na watu kukidhi mahitaji ya kuhamasisha uwekezaji, utalii, masoko, biashara na kadhalika ambapo bajeti ya Wizara peke yake haikidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kabla muda wangu haujaisha niongelee kuhusu, *I mean* mwisho lakini siyo kwa umuhimu, inawezekana leo ni mara yangu ya mwisho kuzungumza katika Bunge hili la Kumi na Mbili nikiwa kama Mbunge wa Kuteuliwa. Utakumbuka kwamba, Rais wetu, Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliniteua Waziri na Mbunge, hivyo niliapa kama Mbunge mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 31 Machi, 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninasimama kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa ya kuwa kwenye Bunge hili kujifunza na kutoa mchango wangu wa Chama changu Cha Mapinduzi na Serikali yetu nikiwa Mbunge *back bencher,* sasa nimetumikia utumishi wa umma kwa ngazi mbalimbali. Ninaamini

nimekusanya uzoefu mkubwa kwenye medani ya siasa na utumishi wa umma ambao utanisaidia kusonga mbele na kuendelea kutoa mchango wangu kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa dakika moja, kama mwanadiplomasia namba moja, kwa kuniwezesha kuteuliwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kuwa Mjumbe Maalum wa Masuala ya Wanawake kuhusu amani na usalama Barani Afrika. Ninapenda pia, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote na Watanzania kwa ujumla kwa salamu zenu za pongezi, kunitakia kila la heri na mafanikio katika majukumu hayo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika sitawaangusha. Ninawaombea wenzangu wote Mwenyezi Mungu awarudishe tena kwenye Bunge lijalo. Kazi na utu, tunasonga mbele, Oktoba tunatiki, Mheshimiwa Rais miaka mitano tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Balozi Mulamula, ndio umeishia hapo hapo? Nikafikiri labda unamalizia mengine? Unaendelea bado?

Basi unga mkono hoja. Nikafikiri ulikuwa na mengine unasema, maana haya mambo, *anyway* tuendelee.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Benaya, Mheshimiwa Mollel.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza ninaungana na wenzangu kuunga mkono kwa asilimia zote bajeti hii ambayo ni mwendelezo wa bajeti zilizopita. Inaenda kukamilisha mambo yote tuliyoyapanga

katika Ilani ya Mwaka 2025. Kwa hiyo, ninaiunga mkono kwa asilimia mi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninaishukuru sana Serikali ya Awamu hii ya Sita chini ya Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaishukuru kwa mambo makubwa iliyofanya katika Jimbo la Mbinga Vijijini. Jimbo la Mbinga Vijijini katika kipindi hiki cha miaka mitano tunajivunia sana uwepo wa Mama huyu kwa sababu, tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya, ndani ya kipindi hiki imejengwa, imekamilika na imeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa hatuna vituo vya afya, sasa hivi vituo vya afya vitano vinafanya kazi. Vilevile, vituo vya afya viwili vimejengwa, upande vimeanza kufanya kazi. Vingine viwili vimepelekewa fedha na vinajengwa, kwa maana hiyo kwa kipindi hiki tutakuwa tumekamilisha vituo vya afya tisa. Kwa kweli, ni jambo la kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kipindi hiki kifupi cha miaka hii minne/mitano zahanati 17 zimejengwa na kufunguliwa, lakini kupitia mapato ya ndani. Hivi ninavyoongea zahanati 16 zimepelekewa fedha, maana yake ni hizi 17 pamoja na 16, zote mpya, zitakuwa zimekamilika ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa shule za sekondari tumefungua sekondari 10 katika kipindi hiki, zote mpya zinafanya kazi kabisa, lakini na zile za nyuma zimepelekewa fedha; baadhi zinajengewa hosteli na baadhi zinakamilishwa maabara, zote hizi zimefanyika ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano. Tumepata shule mpya mbili za msingi, Shule mpya ya Kilango na Shule mpya maalum pale Maguu, ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tunaishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaingia kipindi hiki, Jimbo langu lina vijiji 117, vijiji 96 vilikuwa havina umeme, leo hii vijiji vyote vimepelekewa umeme ndani ya muda huu wa miaka

minne/mitano ya Serikali hii ya Awamu ya Sita. Maana yake ni kuna kazi kubwa imefanyika, kipindi hiki kifupi imefanyika kazi kubwa kwelikweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu hapa ni kwenye upande huu wa umeme, sisi Wanambinga tunatumia sana umeme na tunaoneana wivu wa maendeleo. Kwa hiyo, tukiona nyumba fulani imewekewa umeme na nyumba nyingine haina umeme tunaingia kwenye vita ya maendeleo. Kwa hiyo, kwa sababu vitongoji vyetu viko mbalimbali na tuko nyuma ukilinganisha na wenzetu, ninaomba sana, nimeona kwenye bajeti hii tumetengewa vitu vingi vizuri, kupeleka umeme kwenye vitongoji. Ninaomba sana utekelezaji wa mpango huu wa umeme vitongojini uanze, ili kila kitongoji kwenye Jimbo la Mbinga Vijijini kiweze kufikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile upande wa Barabara. Tulikuwa na shida ya Barabara ya kutoka Mbinga hadi Mbambabay, ilikuwa ni historia, lakini kipindi hiki, mwaka jana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alienda kuifungua Barabara ya kutoka Mbinga hadi Mbambabay, barabara hii sasa inaunganisha mpaka Mtwara. Pale Mbambabay tuna bandari mpya inajengwa na Mtwara kuna bandari kwa hiyo, inaendelea kuifungua Mbinga pamoja na kuufungua Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulikuwa na malalamiko sana kwamba, sisi Wanambinga, sisi Wanaruvuma ni kama tumetengwa, lakini Awamu hii ya Sita imetufungua sisi Wanambinga kwa Barabara, pia imetufungua angani. Tuna uwanja mzuri wa ndege uko pale na ndege zinatua mara kwa mara. Kwa sababu abiria kule ni wengi sana, tunajazana kweli kweli kiasi kwamba, unaomba tiketi unakosa. Ninaomba watu wa *Air Tanzania* waongeze *route,* tuwe na *route* zaidi ya hizo tatu ambazo tunazo, watu ni wengi na wanasafiri kupitia ndege yetu ya *Air Tanzania.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna bandari yetu kule Ziwa Nyasa, kwa maana hiyo usafiri kwa maji kuja hadi Itungi, Kyela,

nao unawezeshwa. Sasa hivi kuna mradi mkubwa kwelikweli wa bandari ya kisasa inayoenda kuunganisha Mtwara na Bandari ya Mbambababay ambayo itawezesha Mkoa wa Ruvuma kufanya biashara kati ya Nchi ya Tanzania na nchi jirani, zikiwemo Msumbiji na Malawi; ni bandari nzuri sana na kazi inaendelea. Ninaipongeza na ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye bajeti hii ya mwaka huu. Bajeti hii tunayoijadili leo ni nzuri kweli kweli. Kama nilivyosema pale mwanzo, kwamba ni mwendelezo wa bajeti zilizopita; ni kweli, kwa sababu tulikuwa tumezoea kule kupata mbolea za ruzuku kwa sababu sisi Wanambinga ni wakulima kweli kweli, bila mbolea hatuvuni, lakini bajeti hii imeweka tena ruzuku. Maana yake ni kwamba tutaneemeka kwa kutumia ruzuku ya awamu ya sita na sasa itaenda awamu nyingine inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti hii pia kumekuwa na punguzo; baadhi ya viuatilifu vimetolewa kodi. Kwa hiyo ni jambo zuri kwa sababu kwenye mikahawa kule na sisi tunatumia viuatilifu. Kwa hiyo kwa kupunguza kodi hii tunakwenda kunufaika sisi Wanambinga kwenye mazao yetu tunayolima. Vilevile pamoja na kodi hii ya ongezeko la thamani. Kwa hiyo kimsingi bajeti hii inakwenda kumtambua Mwanambinga, inakwenda kumtambua vizuri Mwanaruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri kwenye eneo fulani. Eneo la kwanza ni kwamba; bajeti hii tumeweka utaratibu wa kwenda kuweka tozo mpya ya maendeleo ya viwanda *(Industrial Development Levy)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo hili ni zuri kabisa kwa sababu linalenga kuvilinda viwanda vyetu vilivyopo hapa ndani; lakini twende mbele zaidi tujaribu kulipima kama litakwenda kuwanufaisha Watanzania ama linaweza kwenda kuwaingiza kwenye gharama kubwa. Lengo ni zuri, lakini ukienda kiundani kwenye ongezeko hili la kwenye tozo hii mpya hapa ndipo tunapokuwa na malori na ma-*scania* yanayotoka nje, ambayo

kwa mazingira yetu ya Tanzania, kwa mazingira yetu tuliyoyazoea, malori haya ndiyo himilivu, ndiyo yanayotumika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka hii tozo mpya inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama na kuongezeka bei za shughuli za usafirishaji, hali inayopelekea kukwamisha usafirishaji ndani ya nchi. Hivyo basi, ushauri wangu mimi ni kwamba Wizara husika ifanye tathmini kati ya faida tutakazozipata kwa ongezeko hili la tozo mpya na hasara tunayokwenda kuipata kama hii tozo inaendelea kubaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, Serikali ingetathmini vizuri. Ushauri wangu hapo ni kwamba, ikiwezekana tozo hii ingeondoshwa, tubaki kama tulivyokuwa kwa sababu tumeona manufaa zaidi kuliko ongezeko tunaloenda kulipata hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mollel, jiandae Mheshimiwa Mohamed Issa.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi pia ya kuchangia katika bajeti hii. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema yeye ambaye ametupa uzima kwa siku ya leo na tukaweza kuwepo katika Bunge hili, tangu tulipoanza 2020 hadi kufikia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiache kumshukuru Mheshimiwa Rais wangu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anafanya ya kulihudumia Taifa hili na kutufanya sisi tuonekane ni Watanzania hasa katika masuala mengi ya maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na Serikali yote nzima kwa ujumla kwa jinsi ambavyo wanaendelea kufanya kazi zao kwa uaminifu na

uadilifu mkubwa na kufanya mafanikio haya ambayo tunayaona leo yakapata kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninasimama Bunge hili nikielezea mafanikio ambayo tumeyapata katika kipindi cha miaka hii mitano. Nikienda kwenye afya, nilipoingia kama Mbunge nilikuta katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Oltument hakukuwepo kabisa na majengo kama haya; hayafanani hata na kituo cha afya, lakini pale tumeweza kupata kiasi cha shilingi milioni 900 na hospitali ile imebadilika kabisa; Hospital ya Wilaya ya Oltrument ya Wilaya imebadilika kabisa; imejengwa majengo manne na leo wananchi ni mashahidi na hata sasa kazi hiyo imekuwa ni njema na wananchi wanafurahia kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya hospitali hiyo haikuwa nzuri, lakini leo barabara hiyo tumepata zaidi ya bilioni 1.5 ambayo imeweza kutengenezea lami ya kilometa moja na nusu kuelekea kwenye hospitali hiyo. Kwa kweli hongera sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hongera sana Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, haikuishia hapo, kulikuwepo na magofu ya zahanati ambayo ni majengo ambayo hayakumaliziwa ya miaka mingi; lakini kwa kweli imetengenezwa imekuwa nzuri, na wananchi wanafurahia huduma na zimefunguliwa. Kila zahanati imepata. Zahanati ya Leguruki milioni 50, zahanati ya kule Ilkerini wamepata 50, kule Laroi wamepata, kule Oljoro wamepata milioni 50; na maeneo mengi, takriban zahanati kama saba zimekarabatiwa na zimefikia mahali ambapo wananchi wanapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vituo vya afya. Tumeweza kujengewa vituo vya afya takriban vine. Kituo cha Afya cha Oldonyo Sambu tumepata milioni 500 na kinafanya kazi kwa sasa, Kito cha Afya cha Engalaoni kimepandishwa; tumepata pale milioni takriban 870, imebadilika kabisa na ni pembezoni kabisa ambayo inahudumia wafugaji wetu, kule pembezoni wananchi wetu ambao walikuwa mbali sana na hospitali. Leo wanajivunia

matunda ya Serikali yao chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Bwawani tumejenga kituo cha afya cha takriban milioni 603. Tumejenga kituo hicho chini ya Serikali yetu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambapo kwa kweli ni mafanikio makubwa sana katika kipindi hiki. Pia tumeweza kujenga Kituo cha Afya kule Oloiye, kinafanya kazi na wananchi wanapata huduma. Hiki kimejengwa kwa mapato ya ndani. Ninamshukuru pia Mkurugenzi na timu yake nzima kwa kazi kubwa ambayo amefanya, ambapo tumeweza kutumia mapato ya ndani takriban milioni 450.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanatokana na ushirikiano uliopo baina yetu sisi viongozi wote wa ngazi zote kuanzia Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Makonda, Mkuu wangu wa Wilaya, Mheshimiwa Mkalipa, wote hawa tumeshirikiana na Mkurugenzi na timu yake nzima ndiyo maana mafanikio haya ninayoyaeleza hapa yameweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye elimu. Kwenye elimu tumepata mafanikio makubwa sana; kwa sababu ukiangalia tumeshaweza kupata shule tatu mpya. Shule ya Kihutu tumepata zaidi ya milioni 850, sasa hivi inaendelea vizuri watoto wapo ndani; Shule ya Sekondari Mweiga ni mpya tumepata milioni 584, watoto wapo ndani wanasoma. Tumejenga kule Kisongo milioni 584 watoto wapo ndani wanasoma. Haya mafanikio ni makubwa sana kwa kiasi ambacho kila mwenye macho na kila mwenye akili timamu lazima ayakubali na kuishukuru Serikali kwa sababu imefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chote cha miaka mitano pia hakuna wananchi waliosumbuliwa kwa ajili ya kuchanga fedha kujenga madarasa kama wakati ule nyuma. Tumejengewa madarasa yenye thamani ya bilioni 14; fedha ambayo ni nyingi ambayo imeweza kuokoa wananchi kutokuteseka tena kwa ajili ya madarasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye upande wa barabara, ninaishukuru pia Serikali kwa sababu tunayo barabara ambayo inajengwa ya Mianzini – Sambaa – Shangalamtoni, ni barabara yenye thamani ya shilingi bilioni 22. Mpaka sasa wananchi wamefidiwa kiasi cha shilingi bilioni 3.5 na wote wamekwishapata fidia yao. Kwa kweli tunaishukuru Serikali kwa niaba ya wale wananchi, Serikali yetu imefanya kazi kubwa ya kutoa fidia. Hadi sasa mkandarasi yupo kazini, lakini amesimama kidogo kwa sababu hakupata fedha. Kwa hiyo hili ni ombi ambalo ninaliwasilisha kwa Serikali ili iweze kukumbuka barabara hiyo ili mkandarasi huyo aweze kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji miradi inaendelea vizuri. Ombi; tunaomba sasa ile miradi midogo midogo ya maji ambayo haikupata fedha basi Serikali ikakumbuke ili iweze kuhakikisha kwamba wananchi wale wanaweza kupata maji na waweze kufurahia matunda ambayo tayari wameshayaona wao wenyewe kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninarudi jimboni nikiwa na mambo mengi ya kuyasema pale, kwa sababu mengi yamefanyika chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake. Sina wasiwasi kwamba nikisimama jukwaani sina la kusema. Nina mambo mengi ya kusema ambayo hata hapa Bungeni nikianza kuyaeleza kwa sababu ni mengi, mengi sana kiasi ambacho haiwezi kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwa upande wa umeme, tumepata vitongoji 15. Nilipoingia kuwa Mbunge nilikuwa na vitongoji 258; na vitongoji vilivyokuwa na umeme ni kama 102. Hadi sasa tumeshafikisha vitongoji 200, vitongoji ambavyo bado ni 58 tu. Ni kwa kiwango kikubwa sana kwamba Serikali imefanya kazi kubwa ambayo inaamini katika mgao utakaokuja ule uliotangazwa jimbo langu pia litaendelea kupata na vitongoji hivi ambavyo bado vitaingizwa na tutapata umeme. Kwa hiyo kwa kweli tunaishukuru Serikali kwa kazi hii kubwa ambayo imefanyika *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii vile vile tunaipongeza Serikali kwa sababu kwa kitendo cha kupunguza usajili wa pikipiki kutoka 65,000 mpaka sifuri ni kazi kubwa na njema ya kuwafikiria vijana wetu wanaofanya kazi za bodaboda na kazi nyingine; guta kutoka 120,000 mpaka sifuri, lakini na *service levy* nayo imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kweli bajeti hii ninaipongeza kwa sababu imefikiria na kugusa maeneo ya wananchi, ambayo inaleta matumaini makubwa kwa wananchi wetu. Pia ada ya leseni imepungua pia katika bajeti hii; kwa maana ya pikipiki na guta kutoa 70,000 mpaka 30,000. Hayo ni mafanikio makubwa pia kwa vijana wetu wa bodaboda na wengine wote ambao wanafanya kazi hii ya udereva katika bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said, hayupo, amerudi, Dkt. Pallangyo umerudi? Haya changia.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya mwaka wa fedha 2025/2026. Awali ya yote kwa ruhusa yako nitangulize shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu ambaye ametupa afya, uhai na leo tumeweza kukutana hapa; si ajabu itakuwa ni mchango wetu wa mwisho kwa Bunge hili la Kumi na Mbili tukitegemea kwamba Bunge lijalo tutakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa kiwango kikubwa utakuwa ni ushuhuda wa mambo mazuri ambayo Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeyafanya jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kumpongeza Waziri wa Fedha na Naibu wake, Waziri wa Mipango, Naibu wake kwa hotuba nzuri ambazo kwa kweli zinaakisi kazi nzuri ambazo zinafanyika Wizarani; lakini pia zinatuonesha tulipotoka, tulipo na

tunapokwenda. Niwapongeze kwa kazi nzuri sana timu nzima kuanzia Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii kama nilivyosema inaakisi kazi nzuri zinazifanywa na Serikali ya Awamu ya Sita na kwa hiyo moja kwa moja niseme kwamba ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita ambaye kwa kweli kwa miaka miatano ambayo tumekuwa hapa kazi zilizofanyika jimboni ni kubwa mno. Nilisema nitatoa ushuhuda zaidi kwenye mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sekta ya elimu. Jimboni kwangu nimepata shule 11, kumi za sekondari, moja ya amali na moja ya *primary,* lakini ni shule ya mfano. Pia nimepata Chuo cha *VETA* ambacho kipo mbioni kumalizika, tunaamini kwamba siku si nyingi tutaanza kusajili wanafunzi na mambo yatakuwa mazuri jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka sekta ya elimu bado nimepata madarasa mengi sana, madarasa 265; 188 ni ya sekondari. Kwenye sekta ya maji nimepata shilingi bilioni 3.2 kwa kata za Akheri na Nkoarisambu; lakini pia bilioni sita na milioni mia moja kwa Kata za Imbaseni, Maji ya Chai na Kikatiti hadi Maroroni; bilioni 4.1 kwa Kata ya Uwiro kule nyuma ya Mlima Meru. Pia na bilioni 8.2 kwa Kata za Makiba, Gubuni, Shambarai Burka na Kikwe. Hizi si fedha kidogo, ni fedha nyingi sana kwa sekta moja; ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya afya pia tumefanyiwa mambo mazuri ndani ya miaka minne. Tumepata shilingi milioni 900 kwa ajili ya kuboresha hospitali ya wilaya. Tumejenga *OPD* mpya; lakini pia milioni 300 kwa ajili ya *EMD*, kituo cha matibabu ya dharura. Tumepata nyumba ya mtumishi milioni 90. Tumepata vituo vya afya vine; kuna Kituo cha Afya Usa River, kuna Kituo cha Afya Maroroni, kuna Kituo cha Afya Mareu kule King'ori na fedha shilingi milioni 250 zimeshakuja jimboni kwa ajili

ya kituo kingine cha afya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa barabara tulipata shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufungua Barabara ya King'ori ambayo ni ahadi ya Rais kuiweka katika kiwango cha lami. Tuliifungua tukaijenga kwa kiwango cha changarawe na kwa sasa inapitika kwa mwaka mzima. Tunaendelea kukumbushia bwana mipango, Mheshimiwa Waziri wa Mipango tusikie vizuri, Barabara ya King'ori iliahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami; endelea kuifikiria uingize katika mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mbunguni ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara, tulikumbusha hapa kwa hiyo barabara ni muhimu ikajengwa. Barabara hiyo imekwishafanyiwa usanifu na upembuzi yakinifu, lakini kwa bahati mbaya haijawekwa kwenye mpango. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Mpango na Wizara ya Fedha waikumbuke barabara hiyo. Imekwishafanyiwa usanifu, ni ya kutafutiwa fedha ili iweze kujengwa katika kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru tumeendelea kupata fedha shilingi bilioni tatu na milioni mia sita kila mwaka kwa ajili ya barabara zetu zinazopanda milimani. Barabara ya Sagisi kwenda Akeri mpaka Ndobo imekwishajengwa kwa kiwango cha lami kilometa moja. Ninadhani Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameniona, aikumbuke ile barabara ili iendelee kupelekewa fedha ifike milimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo tumepata fedha nyingi, bilioni 10 kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika Kata ya Makiba. Mradi huo unaendelea na tunaamini kwamba muda si mrefu wananchi watakuwa wanafanya kilimo chao bila kutegemea mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye umeme wa *REA* tumepata fedha nyingi. Sasa hivi kuna mkandarasi yupo jimboni anaendelea kufanya kazi ya kusambaza umeme kwa vitongoji 19. Mradi huo

ulianza mwaka jana. Pia tuna ahadi ya vitongoji 29 mwaka huu. Tunaendelea kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kumaliza Bunge hili la Kumi na Mbili. Kipekee kabisa nishukuru wananchi wa Jimbo langu la Arumeru Mashariki kwa kuniamini na kuendelea kuniunga mkono tangu 2020 mpaka leo na kazi nzuri niliyowafanyia, kazi nzuri Serikali iliyowafanyia ninadhani watanipokea vizuri; mwezi Novemba tuonane tena hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kukutakia wewe heri, ninakutakia kila la heri. Tunakwenda kwenye kampeni siku si nyingi; wananchi wale kwa kazi ambayo unawafanyia wakurudishe hapa, pamoja na Mheshimiwa Spika mwenyewe, lakini pamoja na Wabunge wenzangu na Mawaziri wote kama tulivyo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache. niseme ninakushukuru sana kwa muda huu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulamula ameomba kumtangaza mgeni wake; Mhariri mahiri Rajab Yassir Ramadhani wa *Star City* Dodoma. Yupo? Mheshimiwa Mulamula, ametangulia *canteen* utakutana naye kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti Kuu hii na kwanza nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia afya na uzima na kuendelea kuwatumikia wananchi waliotuleta katika jumba hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipenzi chetu, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu vizuri akisimamia shughuli za

maendeleo yanayokuja hatua kwa hatua tena kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Mawaziri wetu wawili; Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na wasaidizi wao mahiri ambao wako hapa ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kutuwekea sura halisi ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nianzie mahali ambapo kama mtu niliyelelewa na chama makini Chama Cha Mapinduzi nisiposema nitaona siitendei haki nafsi yangu. Ninataka niwakumbushe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, baada ya uhuru wa nchi yetu mwaka 1961 na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwaka 1964 tuliendelea na kazi ya kujenga nchi mpaka leo na kazi hii ya kujenga nchi sisi hatutaimaliza. Sisi tutafanya kwa kiasi chetu na wengine watakuja watafanya na wengine watakuja watafanya. Hata katika Mataifa hayo yaliyoendelea bado wanaendelea na kazi za kujenga nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamaanisha nini? Tunapofika mahali tukasema hatumdai Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, hatumaanishi kwamba kazi ya kujenga nchi imekwisha. Hapana, ila tunamaanisha yale malengo yaliyowekwa na Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025 amefanikiwa kuyakamilisha na mengine amepita kiwango cha kukamilisha. Kwa hiyo, hii tafsiri isije ikachukuliwa kwamba hatumdai. Hapana, ni kwamba tunasema hatumdai kwa sababu yale malengo yaliyowekwa kwenye Ilani kabisa kabisa ameyakamilisha na mengine amekwenda amevuka hata kiwango cha kukamilisha. Kazi ya kujenga nchi bado ipo na wananchi wangine wanaokuja hata sisi tukiondoka duniani wataendelea na kazi ya kujenga nchi kwa sababu kazi ya kujenga nchi ni kazi endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema hapa kwamba tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu, kwa sababu Rais anayejali watu anaonekana katika mambo ya msingi yanayohusu maisha ya watu. Ni chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais huyu

tumeboresha elimu kwa kiasi kikubwa na kuondoa ada kutoka elimu ya msingi mpaka kidato cha tano na sita. Pia, tumeongeza mikopo katika elimu ya juu kupitia kwa Rais huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mheshimiwa Rais huyu pia tumeboresha huduma za afya. Leo hospitali za mikoa karibu zote zina *CT scan machine*. Hospitali za mikoa karibu zote watu wanafanyiwa *dialysis*. Ukiwa na matatizo ya figo sasa hulazimiki kuhama kwenye mkoa wao uende Dar es Salaam ukaishi. Utakaa mkoani kwako kwa sababu vifaa hivi Mheshimiwa Rais huyu kaleta katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais anayejali watu ameongeza kiwango cha upatikanaji maji mijini na vijijini kiasi ambacho leo tatizo la maji kwa sehemu nyingine limekuwa ni hadithi. Rais anayejali watu ameongeza upatikanaji wa umeme. Leo Mkoa kama wa kwangu Kigoma ambao tangu Tanzania imekuwa Jamhuri ulikuwa haujaungwa na Gridi ya Taifa, mkoa mzima sasa umeungwa na Gridi ya Taifa. Kwa nini tusimpe maua yake Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais anayejali watu ameongeza na kusimamia suala la upatikanaji na utumiaji wa nishati safi ili kuwakinga akinamama na madhara yatokanayo na nishati chafu ya kupikia. Huyu ni Rais anayejali watu. Rais anayejali watu ameendelea kusimamia Mfuko wa *TASAF* ili kusaidia watu wenye familia ambazo ziko katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapofika kwenye haya na mengine mengi ambayo muda wa kuyataja haupo, ndiyo tunaposema Mheshimiwa Rais huyu ni Rais wa mfano na anastahili kupewa maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kwangu kuna mambo makubwa sana yamefanyika. Hili la umeme nimelisema, lakini sisi tulikuwa na tatizo kubwa la barabara inayotuunganisha sisi na Mkoa wa Kagera, yaani kutoka Kigoma kwenda Nyakanazi na barabara inayotuunganisha sisi na Mkoa wa Tabora yaani kutoka Kigoma kuingia Tabora. Leo ninavyozungumza kazi hizi

zimefanyika. Barabara ya Tabora – Kigoma sasa hivi iko kwenye 98%, imebakia kama kilometa 17 tu wamalizie kuweka lami. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachokusudia kusema ni kwamba, hali ya jimboni kwangu na majimbo mengine nchini inatia matumaini kiasi ambacho kinatupeleka sisi Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kifua mbele kwa wananchi kuomba ridhaa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nizungumze jambo moja kupitia bajeti iliyowasilishwa. Nalo ni suala la marekebisho ya Sheria ya Uingizaji Bidhaa Nchini, Sura ya 276. Nimemsikia hata mwenzangu Benaya ameligusia jambo hili nami ninaomba niligusie. Hapa ninatoa tahadhari kubwa kwa sababu sisi kama nchi moja ya watu ambao wanatuhangaisha kuhakikisha kwamba maisha yao yanaboreka ni wakulima na wafugaji wa nchi hii. Hawa ndiyo moja ya watu ambao tunahangaika nao kwa kiasi kikubwa na hawa wakulima tatizo lao siyo tu kulima, tatizo lao kubwa liko katika usafirishaji wa mazao yao kuyafikisha sokoni ili waweze kusafirisha mazao hayo ni lazima watumie barabara na lazima watumie magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wameweka kitu kinaitwa *industrial development levy* 10% na mnataka hii itozwe kwenye bidhaa zinazotoka nje ikiwa ni pamoja na magari ya *transport* kama vile ma-*Scania, Leyland* ndefu hizi, sijui mafuso. Sasa hii wataenda kuongeza gharama kubwa ya usafirishaji na kwa maana hiyo kufanya uwepo mzigo mkubwa sana kwa watumiaji na walaji. Kwa mfano, leo hii mzigo unaotoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa kutumia usafiri wa magari unachajiwa kilo moja kati ya shilingi 250 hadi 260 lakini kwa kuongeza hii kodi, mzigo huu utakwenda utafika mahali hata shilingi 300 au 300 na kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivi utatokea mfumuko mkubwa wa bei ambao sasa hivi tunao kile Kigoma, watatuongezea kutokana na kodi hii. Ninawaomba sana, ninawaamini Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, wakae

waangalie jambo hili. Jambo hili haliendi kumgusa tu yule aliyeagiza bidhaa lakini linakwenda kufika mahali linamgusa yule mwananchi ambaye ndiye anategemea kupata manufaa yatokanayo na usafirishaji wa bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumza ni suala la *liquidity* kwenye benki zetu. Ndugu zangu lazima tuambiane na tuwaombe Wizara ya Fedha, wakae na Wizara ya Biashara na Wizara nyingine wazungumze. Sasa hivi lipo tatizo la wananchi wengi kutokupenda kupeleka fedha benki. Katika kila shilingi 10 ni shilingi tatu tu ndiyo inayoonekana katika mfumo ulio rasmi yaani kwenye *mobile wallet*, hizi *M-Pesa* na nyingine na kwenye benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa nyingi ziko mikononi na utaona tu hata yakipatikana majanga ya moyo au jengo limeanguka wananchi wanalia mara mbili. Unakuta mtu anasema nilikuwa na milioni 200 na bilioni 300. Tujiulize kwa nini watu hawataki kupeleka pesa benki? Watu hawataki kupeleka pesa benki kutokana na tozo na kodi. Hebu waangalie jambo hili ili liweze kutuweka mahali pazuri na benki zetu sasa zimefika mahali kwa kukosa *liquidity* zina-*invite* watu kuweka *fixed deposit* na wanatoa riba mpaka 15%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama benki inatoa riba kwa mtu 15% kuweka *fixed deposit,* huyo anayekopeshwa na hiyo benki atatozwa asilimia ngapi? Hili ni tatizo. Ninaiomba sana Wizara ya Fedha ni watu ambao ninawaamini, kuna vichwa viko hapo; Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake ni watu makini sana, wakae wa-*harmonize* hii hali. Pesa ziingie benki. Benki zipate *liquidity* ili ziweze kukopesha na hapo ndiyo tutakapopata maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, hata suala zima la kodi, kadri wanavyokuwa na pesa nyingi hata waichaji kidogo watapata fedha nyingi, lakini sasa hivi wanachaji tu kwenye ile shilingi tatu kwenye kila shilingi 10, lakini waki-*harmonize* zikaja pesa za kutosha maana yake watatoza kodi na watapata fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyoyasema ninaomba kuunga mkono hoja ya bajeti hii nzuri kwa manufaa ya wananchi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Niwashukuru kwa michango mizuri. Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.50 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 20 Juni, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*